# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 21 Juni, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe.* Mussa A. Zungu*) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017 (*The Finance Bill, 2017).*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE – (K.n.y. MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017 (*The Finance Bill, 2017).*

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017 (*The Finance Bill, Act* 2017).

**MWENYEKITI**: Ahsante, Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 426

### Kuboresha Maslahi ya Madiwani Nchini

**MHE. KISWAGA B. DESTERY** aliuliza:-

Madiwani ni wasimamizi wakuu wa rasilimali za halmashauri na wakati wa uchaguzi wa Madiwani, Wabunge na Rais ni mafiga matatu:-

(a) Je, ni lini Serikali itawaongezea posho ya mwezi Madiwani hao?

(b) Je, ni lini Serikali itawapa usafiri na msamaha wa kodi Madiwani katika vyombo vya usafiri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Waheshimiwa Madiwani

katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Serikali ilipandisha posho za Madiwani kwa mwezi kutoka Sh.120,000/= hadi Sh.250,000 kupitia Waraka Maalum wa tarehe 16 Agosti, 2012. Vile vile katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 posho hiyo iliongezwa kutoka Sh.250,000/= hadi Sh.350,000/= kwa mwezi kwa Madiwani na Sh.400,000/= kwa mwezi kwa Mwenyekiti au Meya. Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya Waheshimiwa Madiwani kadri hali ya uchumi wa nchi inavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Waheshimiwa Madiwani kupewa vyombo vya usafiri na msamaha wa kodi, kwa sasa Serikali imeridhia Waheshimiwa Madiwani wakopeshwe na Mabenki kwa masharti nafuu kutokana na posho zao. Tayari mabenki yameanza kutoa mikopo kwa Waheshimwa Madiwani zikiwemo Benki za *NMB* na *CRDB*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwamba uchumi ukiwa nzuri tutaongeza, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa majibu yanaonesha kwamba kila baada ya miaka miwili Serikali ilikuwa ikiongeza posho za Waheshimiwa Madiwani mpaka 2015 na leo tuko 2017 tayari miaka miwili. Je, Serikali haioni kwamba kulingana na mazingira wanayofanyia kazi Waheshimiwa Madiwani pamoja na kupanda kwa maisha, sasa ni muda muafaka wa kuongeza posho angalau kidogo ili waweze kumudu maisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mikopo hii wanayokopa kwenye mabenki ni kutokana na posho yao, Serikali haioni kwamba hizi fedha ni ndogo zaidi, hawawezi hata kupeleka kwenye usafiri. Je, Serikali kwa nini isiweke ruzuku kama inavyotoa kwa Waheshimiwa Wabunge nusu ili Waheshimiwa Madiwani waweze kumudu usafiri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba kwa wastani wa miaka miwili posho ya Madiwani inaongezeka; naomba nikiri kwamba Madiwani wetu wanafanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Kiswaga na Waheshimiwa Wabunge naomba niwaambie kwamba kwa bahati nzuri nilipata fursa ya kukaa na Madiwani katika vikao vya *ALAT* kule Musoma na hapa Dodoma na hii imekuwa ni *concern* yao kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni kweli na sasa hivi limewasilishwa katika mamlaka husika na kwamba sasa linafanyiwa kazi na linachambuliwa vizuri. Mambo yakikamilika vizuri basi watapata mrejesho kwamba Serikali imeamua vipi katika jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ruzuku kwa vyombo vya usafiri nadhani ni wazo zuri naomba tulichukue, na Serikali itaangalia ni jinsi gani itafanya kwa sababu Madiwani wanafanya kazi kubwa, lakini siwezi kutoa *commitment* kutoka hapa kwamba nini kinafanyika kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Kapufi, Mheshimiwa Lubeleja na Mheshimiwa Kange.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri hapa amesema wataongeza kipato kwa Madiwani ikiwa mapato ya Serikali yataongezeka; lakini kwa mwaka sasa Serikali imekuwa ikitangaza kuongezeka kwa mapato, yaani makusanyo yamekuwa makubwa, ninachokitaka badala tu ya kuwalipa posho kwa nini sasa Madiwani wasilipwe mishahara kama tunavyolipwa sisi Wabunge ili wafanye kazi hiyo kwa moyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Menyekiti, Mheshimiwa

Mwenyekiti, wazo la kulipwa mshahara na posho; kwa sababu kuna nafasi mbalimbali zimetengwa kwa utaratibu wake; kwa utaratibu Madiwani wanalipwa posho sawasawa na Wenyeviti wa Vijiji, kwamba kuna posho ile ya asilimia 10 kwa Wenyeviti wa Vijiji, lakini kuna posho maalum ya Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wazo la mshahara, hili tuseme ni wazo tu ambalo Wabunge wanatoa kuona jinsi gani jambo hili linaboreshwa. Hata hivyo, mara nyingi Serikali inafanya tathmini katika maeneo mengi zaidi na hasa kuangalia *wage bill* ya Serikali itakuwaje baadaye endapo Madiwani wataingizwa katika eneo hilo kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo nasema kwamba ni mawazo au chemchem ambayo inasaidia kuboresha ili unapofika wakati tuangalie jinsi ya kufanya; lakini kwa sasa hivi utaratibu tunaokwenda nao ni utaratibu wa posho kwa mujibu sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Huko nyuma Serikali ilikuwa ikitoa mafunzo kwa Madiwani ambapo mafunzo hayo yaliwajengea uwezo mkubwa ikiwa ni pamoja na kufahamu mipaka yao. Je, ni lini Serikali itarejesha mafunzo haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hilo swali ni lingine, lakini lijibu kwa sababu ni muhimu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kwa kipindi cha nyuma kulikuwa na mafunzo ya Madiwani ambayo yalikuwa yakitolewa ili kuwajengea uwezo waweze kufanya kazi yao vizuri kwa sababu wao ndio wanafanya maamuzi katika Mabaraza yetu ya Madiwani katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hapa katikati mafunzo kidogo yalisimama. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato huu wa mafunzo umeanza katika maeneo mbalimbali na mafunzo haya yataweza kuwafikia Madiwani, lengo kubwa ni kujenga uwezo wao kwa kadri itakavyoonekana kwamba itafaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje, jiandae Mheshimiwa Kange na Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo. Bahati nzuri mimi nimekuwa Diwani kwa miaka kumi na tano na Mwenyekiti wa Halmashauri. Kazi ya Udiwani zamani ilikuwa mikutano tu, unakuja kuitwa kwenye kikao unarudi nyumbani; lakini kwa kuwa sasa hivi Udiwani ni kusimamia miradi, ikianza kujengwa darasa mpaka jioni uko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba mtekeleze yale maagizo au maelekezo ya Tume ya Lubeleje ya kushughulikia maslahi ya Madiwani, muwalipe Madiwani posho ya kutosha ili nao waweze kumudu maisha kwa sababu wanashinda kwenye miradi mpaka jioni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mbunge wa siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri wazi kwamba kuna Tume iliundwa ambayo Mheshimiwa Lubeleje ambaye ni Mbunge; ndiyo maana namwita *Senior MP* alikuwa ndiye Mwenyekiti wa Tume ile. Tume ile ilitoa mapendekezo mbalimbali na miongoni mwa mapendekezo hayo yaliyotolewa katika Tume ya Lubeleje ndiyo haya yaliyosababisha kufanya maboresho ya hata hivi viwango tunavyoviona hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kikubwa zaidi na tukiri wazi kwamba Madiwani ndio wenye jukumu kubwa sana la kusimamia kazi za kule *site*. Ndiyo maana nimesema kwamba Serikali inalitazama hili kwa upana wa hali ya juu; kwamba nini tufanye. Kwa hiyo, hali itakapokuwa imeridhisha na maamuzi yakifanyika naamini kwamba posho ya Madiwani itaongezeka. Lengo ni kuwawezesha kufanya vizuri katika usimamizi wao wa kazi kwani wanafanya kazi kubwa na hakuna mtu anayebeza katika hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kange, ajiandae Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. KANGI A.LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Waheshimiwa Wabunge hapa kila tukigusa maombi ya fedha kwenye miradi ya maji, barabara na afya tunaambiwa pale hali ya uchumi itakapokuwa nzuri. Leo pia tunagusa suala la posho za Madiwani tunaambiwa hali ya fedha itakapokuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye bajeti hii anasema hali ya uchumi ni nzuri na kwenye ukurasa wa tatu wa taarifa ya Benki, hii hapa ninayo, wanasema uchumi umekuwa kwa asilimia saba, ni kiwango kikubwa sana cha kimataifa. Sasa je, hii hali ya uchumi wanayotaka ni asilimia ngapi ndiyo hali ya uchumi itakayokuwa nzuri? Mimi nashindwa kuelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza hali ya uchumi itakapokuwa nzuri; ni kweli tunakwenda vizuri, lakini malengo ya Serikali hii ya Awamu ya Tano ni kwenda mbali zaidi na ndiyo maana najua suala hili la posho si kwa Madiwani peke yake ni hata Walimu pamoja na watumishi wengine, kila mtu anataka angalau mshahara wake uweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tumesema kwamba acheni Serikali kwanza ijipange vizuri katika hili. Tunajua tuna vipaumbele vyetu vingi sana ambavyo ni lazima vyote tuvitekeleze. Ngoja tujipange vizuri, lakini kila kundi litaweza kufikiwa kwa kadri Mheshimiwa Rais alivyojipanga na Serikali yake ya Awamu ya Tano na hatimaye kila mtu *ata-realize* kwamba kweli hatukufanya makosa katika kupanga mipango muafaka kwa ajili ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na posho za Madiwani, Wenyeviti ya Vijiji na Vitongoji kuwa ndogo, lakini bado halmashauri nyingi zimekuwa zinawakopa viongozi hawa posho hizi kiasi kwamba wana muda mrefu hawalipwi. Sasa Serikali iko tayari kutoa kauli yenye muda maalum kuhakikisha kwamba viongozi hawa wanalipwa madeni yao ya posho zao? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, juzi nilipokea *concern* kutoka Buchosa kwamba Madiwani wamekopwa takribani miezi minane, hili halikubaliki hata kidogo. Wakati mwingine utagundua kwamba ni uzembe tu wa usimamizi nzuri. Watu wanafanya *collection* lakini wakati mwingine katika suala la kuwalipa Madiwani wanaona kama ni hisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe maelekezo kwamba halmashauri mbalimbali tunafanya makusanyo, makusanyo yale yanakusanywa na Madiwani ndio wanaofanya maamuzi, lazima mwende mkalipe posho za Madiwani kwa kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wanafanya kazi kubwa lakini posho zao hazilipwi na wakati huo huo shughuli nyingine zinaendelea ambazo Madiwani hao ndio waliosimamia kupata fedha hizo, haitokubalika. Tutaenda

kufuatilia halmashauri moja hadi nyingine. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tuta-*cross check* na halmashauri mbalimbali ambazo kwa makusudi kabisa wamekataa kuwalipa madiwani *either* kwa kiburi au kwa jambo lingine lolote.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi hiyo hiyo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Almasi Maige.

Na. 427

**Bwawa lililojengwa na TASAF**

**MHE. ALMAS A. MAIGE** aliuliza:-

Katika Kijiji cha Majengo, Kata ya Ikongolo, *TASAF* ilijenga bwawa kubwa la kukinga maji ya mvua kwa madhumuni ya umwagiliaji na matumizi ya vijiji vyote vinne vya Kata ya Ikongolo, lakini bwawa hili lilivuna maji kwa mwaka mmoja tu na kisha kwa masikitiko makubwa bwawa hilo lilipasuka kingo yake moja na maji yote yakatoka:-

(a) Je, wataalam wa Serikali wamegundua ni kwa nini bwawa hilo limepasuka kingo yake kuu?

(b) Kwa vile bwawa hilo lilileta shughuli nyingi za kiuchumi kwa wananchi kwa kilimo cha umwagiliaji, je, ni lini Serikali itaanza harakati za kuziba mpasuko uliotokea katika kingo za bwawa ili wananchi waendeleze shughuli zilizosimama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora kaskazini lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kubomoka kwa tuta *(Embarkment)* la Bwawa karibu na sehemu ya kupumulia *(spillways)* katika Kijiji cha Majengo kulitokana na athari za mvua nyingi zilizonyesha msimu wa mwaka 2013/2014.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa bwawa hilo, Serikali imeidhinisha shilingi milioni ishirini kwa ajili ya ukarabati wa bwawa hilo ambao utahusisha ujenzi wa njia ya kuchepusha maji *(spillways).* Fedha hizo zitatokana na ruzuku ya maendeleo kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siridhiki kabisa na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, na huu ndio mzaha ambao hatupendi Wabunge. Milioni 20 mimi ninazo mfukoni hapa, si ningetengeza bwawa hilo? Halitengelezeki kwa milioni 20 bwawa hilo, Bwawa kubwa na limepasuka. Nataka kujua na alisema kwamba itatokana na ruzuku, nani anatoa ruzuku, hatujui; lakini hela zinakwenda kwa nani, hatujui; mkandarasi nani atafanya hiyo kazi hatujui, jibu hili si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki tena kuomba mwongozo baadaye lakini ningependa Waziri anijibu vizuri, kwamba hizo hela zitatoka wapi na hela hizo hazitoshi, lakini je, lini hela zitapatikana? Hiloni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tangu mwaka 2014/2015, 2016/2017, leo miaka mingapi? Barabara imejaa miti iliyoota, nani atatengeneza hiyo barabara ya kwenda kwenye bwawa kwa sababu haipitiki? Nataka kujua pia je, barabara ile itatengenezwa na nani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu milioni ishirini; mara nyingi kila mtu ana taaluma yake. Maana yake

ma-*engineer* kama wamefanya *assessment;* kwa sababu ni ile sehemu iliyobomoka tu. Kama Mbunge anahisi kama shilingi milioni ishirini haitoshi; katika hili naomba niseme kwamba; kwa sababu bwawa limevunjika katika *spillways;* ngoja tupeleke hizo fedha halafu tuone nini kitaendea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapofanya *assessment;* kama mtaalam wa maji, mabwawa, *engineer* amefanya *assessment* na amesema ni milioni ishirini, lakini Mheshimiwa Mbunge anasema haitoshi, aah, tutaangalia maana huyo mtu inawezekana *qualifications* zake hazimtoshi kukaa katika nafasi hiyo, ndiyo maana ameleta *assessment* ya milioni ishirini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili maana yake si kwa sababu yuko Jafo hapa; kwa sababu kuna mtu alifanya *designing* na *assessment* ya bwawa lilivyopasuka na amesema milioni ishirini. Isipotosha maana yake watu hawa ndio watakaokuwa wanakwamisha shughuli za maendeleo katika maeneo yetu, hatutaweza kuvumilia. Naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwa sababu nina safari ya kwenda Kaliua na Urambo nitapita kwenda kutembelea bwawa hilo na kuangalia hali halisi ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini fedha hizi zitatoka katika *Local Government Capital Development Grant* kutoka TAMISEMI, naomba asihofu fedha hizo zitakwenda. Kuhusu suala la barabara kufika katika eneo lile naomba niseme kwamba hiki ni kipaumbele cha Halmashauri yenyewe kadri inavyosema kwamba bajeti yake inajenga barabara katika eneo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naamini kwamba tutafika *site* tutakwenda kuiona hiyo barabara, basi waweke kipaumbele kama barabara hiyo ambayo haipo katika mpango lazima iwekwe katika mpango ili wananchi waweze kufika katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massare, ajiandae Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo tu la nyongeza. Matatizo yaliyoko huko Uyui yapo pia katika Jimbo la Manyoni Magharibi. Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kuna mabwawa madogo yale malambo madogo ambayo yamepasuka na mengine yamefukiwa na maji likiwemo la Kaskasi stesheni, Mkalamani Itigi Majengo, pamoja na la Muhanga. Je, Serikali iko tayari na sisi kutusaidia fedha kidogo katika Mfuko huo ili na sisi kama halmashauri tuweze kurekebisha mabwawa haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Anataka Mfuko tu usimpe tena, maana wewe mtaalam wa hiyo Wizara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ame-*pose* hilo swali hapa sasa hivi na hatujui kwamba mabwawa hayo *assessment* imefanyika na inahitaji gharama kiasi gani na hatujui kama Halmashauri imeweka kipaumbele gani katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa sababu suala la mabwawa hayo ni jambo la msingi; naomba tuwaagize wenzetu wa Halmashauri ya Itigi, kwamba sasa wataalam wa maji waweze kwenda katika eneo hilo wafanye tathmini ya mabwawa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu mabwawa haya yakijengwa yataisaidia jamiii katika eneo letu; tujue kwamba kama Serikali tunajipanga vipi kurekebisha mabwawa hayo mara baada ya kupata bajeti halisi na tuweze kuliweka katika mipango ya maendeleo ya bajeti katika Halmashauri ya Itigi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe, wajiandae Mheshimiwa Ungando na Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Matatizo yaliyopo Uyui kwenye miradi inayosimamiwa na *TASAF* na TAMISEMI yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Jimbo la Ndanda hasa kwenye Kata ya Mwena.

Mheshimiwa Mwenyekit, kwenye hii TAMISEMI *phase III* ambayo imekuwa ikishirikisha wananchi. Kuna miradi pale ya mabomba ambayo Mheshimiwa Diwani kwa kushirikiana na watendaji wamekuwa hawatekelezi wajibu wao; kwa maana ya thamani ya pesa haionekani kwenye miradi. Sasa Mheshimiwa Waziri tunaomba atuleze badala ya kusubiri mpaka haya mambo yaharibike kabisa ndipo Wizara yake ikachukue hatua, je, hawaoni kuna haja ya kufuatilia utoaji na matumizi ya pesa ya *TASAF* katika maeneo mbalimbali kadiri siku zinavyokwenda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme wazi kwamba jambo la kusimamia fedha *(value for money)* katika maeneo yetu naomba tulipe kipaumbele sana. Mheshimiwa Cecil nakumbuka tumetembelea mpaka kwenye bwawa lake pale chini. Kama fedha lakini usimamizi si mzuri na kama fedha imekwenda wengine wanatengeneza *caucus* kule kwa ajili ya kula ile fedha, jambo hilo halikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wao ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha, wasikubali kupitisha mradi wa aina yoyote katika *site* na Majimbo yao ambayo wanaona katika njia moja au nyingine, mradi huu baadhi ya watu wanahujumu kwa makusudi. Tukifanya hivi ndipo tutalinda fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa naomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Masasi, kwamba aangalie kwanza nini kilichotokea katika mradi huo ambao tunasema kwamba lengo ni kuweza kuwasaidia

wananchi halafu tupate taarifa. Nitaenda kufanya *follow up* ya haraka ili fedha zinapokwenda kule *site* lazima fedha zile ziweze kuleta matunda makubwa sana kwa manufaa ya wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ungando, ajiandae Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba niulize swali la nyongeza. Kutokana na mvua zilizonyesha, barabara yetu ya kutoka Mbwela kwenda Muholo imeharibika zaidi. Je, Wizara yake ina mkakati gani wa kutukarabatia barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Haya, mtaalam wa Wizara, naona hapa kazi tu mzee.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Ungando amehamisha goli lakini ngoja nimjibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, ile barabara kwanza ni korofi na Mheshimiwa Mbunge anakumbuka siku ile tulikuwa *delta* mpaka usiku saa mbili ndipo tulirudi kwa kuwa barabara iliharibika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumepitisha fedha za barabara za vikwazo na barabara hiyo tumeiweka basi nimhakikishie Mheshimiwa Ungando kwamba kwa sababu bajeti tumeipitisha jana na yeye amepiga kura ya ndiyo, bajeti hii sasa itakapoanza kufanya kazi katika eneo lake lile tutalipa kipaumbele ili barabara ile tuirekebishe sambamba na ujenzi wa yale madaraja ambayo yanakwamisha sana kuwapitisha wananchi wa Kibiti.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. WILLY Q. QAMBALO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tatizo la mabwawa kupasuka lililopo Tabora Kaskazini linafanana kabisa na matatizo tuliyonayo kule Karatu. Bwawa la Bashay lililopo nje kidogo ya Mji wa Karatu lilikuwa chanzo muhimu sana cha maji kwa wakazi wa Kata ya Qurus hadi pale lilipopasuka wakati wa zile mvua za *el-nino*. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati bwawa hilo ili wananchi wa Gongali, Bashay na Qurus waweze kupata huduma hiyo muhimu ya maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Mipango yote ya Serikali lazima ianze katika Halmashauri zetu, tufanye *needs assessment,* tubainishe na tuweke katika mipango ya Serikali. Hata hivyo, imeonekana kwamba katika maeneo mengi mabwawa haya mengi sana yanapasuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasihi hasa Waheshimiwa Wabunge tunaposimama katika maeneo yetu, japo kuwa si wataalam sana katika maeneo hayo lakini tuna haki ile miradi wakati inajengwa tuisimamie kwa karibu kwa sababu wakati mwingine wakandarasi wanapojenga ile *embarkment* haishindiliwi vizuri na hatimaye lile tuta linapasuka au *spillway* ya kupitisha utoro wa maji haiwi vizuri na mwisho wa siku maji yanafurika na bwawa linapasuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa ndugu yangu Mbunge wa Karatu jambo hili tumesema kwamba kama Serikali tumelisikia, lakini naomba nielekeze kama nilivyotoa maelekezo katika maeneo mengine, kule Halmashauri ya Karatu tuweke kipaumbele cha kufanya ukarabati wa bwawa hili ambalo linasaidia wananchi ili hatimaye tutenge fedha katika bajeti ile ili tuweze kurekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba niseme kwamba tumelisikia, tumelipokea na kama Serikali tunajua kuna wananchi wetu huko wanapata shida kwa sababu bwawa limepasuka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa mabwawa yameendelea kupasuka katika nchi hii na kwa kuwa katika Wilaya ya Monduli, Kata ya **Esilalei, bwawa la Josho na Oltukai,** tulishaleta mpaka kwa Waziri Mkuu kuomba Serikali iweze kukarabati mabwawa yaliyopasuka mwaka 2015. Je, ni lini Serikali itakuja kukarabati mabwawa haya ambayo Serikali ilishahaidi kuyakarabati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ukiangalia kila mtu anazungumza kuhusu bwawa lililopasuka na nimetoa maangalizo, kwamba mabwawa haya yanapasuka huenda kandarasi haikusimamiwa vizuri, ile *spillway* (utoro wa maji) haukuwa vizuri au ile *embarkment* haikushindiliwa vizuri au utaalam wenyewe uliotumika huenda haukutumika sawasawa; kwa hiyo hapa inawezekana kila mtu atazungumza bwawa lake limepasuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelekezo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote wafanye tathmini ya mabwawa yote yaliyopasuka ili Serikali tuone kwamba tuna tatizo kiasi gani tuweze kulipangia mpango na tulirekebishe na hatimaye mabwawa haya yawasaidie wananchi katika mifugo, maji ya kunywa na matumizi mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri, Mheshimiwa Maria Ndila Kanyoye.

Na. 428

**Bwawa Lililojengwa na TASAF Kata ya Ikongolo**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Serikali imeziagiza Halmashauri zote za Wilaya nchini kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya vijana na wanawake:-

Je, Serikali imetoa kiasi gani kwa vikundi vya vijana na wanawake tangu zoezi hilo lianze?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2010 – 2016 Serikali imefanikiwa kutoa shilingi bilioni 122.4 kwa ajili ya mikopo ya vijana na wanawake ambazo zinatokana na asilimia kumi iliyotengwa kila mwaka kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imepanga kutoa shilingi bilioni 56.8 ambapo mpaka mwezi Machi 2017 zimeshapelekwa shilingi bilioni 17.3 kwenye vikundi vya wanawake na vijana. Serikali itaendelea kutenga fedha hizo kila mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imeshatenga shilingi bilioni 61.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangoye.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya wanawake na vijana hususan wa Mkoa wa Mwanza napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa kumekuwa na tabia ya baadhi ya Halmashauri za Wilaya kutokutoa asilimia kumi

kwa wanawake na vijana kikamilifu na nyingine kutokutoa kabisa; je, Serikali inachukua hatua gani juu ya Halmashauri hizi zinazokaidi agizo hili la Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa vikundi vya maendeleo vya wanawake na vijana vimekuwa ni vingi sana na fedha hii imekuwa ikinufaisha vikundi vichache; je, ni lini Serikali itaongeza asilimia hii ili iweze kunufaisha vikundi vingi na ukizingatia kwamba ikifanya hivyo itakuwa imepunguza kwa asilimia kubwa tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mbunge kwa harakati zake kama kijana na kama mwanamke kugombea na kupambana kwa haki za wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu suala la asilimia kumi, kwamba Halmashauri nyingine hazitengi; katika bajeti ya mwaka wa 2016/2017, tulipotenga bilioni 56.8 tulitoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote kwamba *commitment* ya bajeti ya Serikali katika *10 percent,* yaani *five* ya vijana na *five* ya akinamama lazima itekelezwe. Katika hili tumeona kwamba mpaka mwezi Machi tumetoa bilioni kumi na saba, lakini mpaka juzi wakati tunafuatilia ina maana fedha zinaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwasihi hasa Waheshimiwa Wabunge, sisi ni wajumbe katika Mabaraza yetu, fedha zile zinakusanywa wala haziendi kwa Mpango haziendi Hazina, zinaishia katika Halmashauri zetu. Lazima kila kinachokusanywa kila mwezi tunapoingia katika Kamati ya Fedha tusikubali kupitisha ile bajeti, fedha zimekusanywa pale, lazima tutenge moja kwa moja *five percent* ya vijana na *five percent* ya akinamama ili tuwasaidie watu wetu kule *site.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Wakurugenzi wote ambao tumekubaliana lazima walitekeleze na tarehe 30 mwezi wa sita tutafanya *assessment* ya Wakurugenzi wote ambao wameshindwa ku-*meet commitment* hii ambayo ilikuwa ni *guideline* na maelekezo ya Kamati ya TAMISEMI ya Bunge hili wakati tunapitisha bajeti. Kwa hiyo wakurugenzi wote lazima wajiandae, hiyo ni miongoni mwa *assessment* tutakayoifanya katika *performance* ya kufanya kazi zao katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuongeza *ten percent;* naomba nimwambie dada yangu, hii *ten percent* yenyewe inatosha kwa sababu fedha zile kuna nyingine zinakwenda katika maendeleo, posho za Madiwani na posho ya vijiji. Asilimia kumi kinachotakiwa ni *compliance* tu, kama kila Halmashauri itaweza kutoa kweli asilimia kumi tutaweza kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba asilimia kumi inatosha, isipokuwa sasa lazima wajue tumetoa maelekezo kwamba katika ile asilimia kumi lazima watenge asilimia mbili kwa ajili ya walemavu katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo, wajiandae Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Raymond.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa vijana wanaohitimu elimu ya sekondari katika nchi yetu ni kama 400,000 hivi na wanaokwenda kidato cha tano ni kama vijana 90,000, zaidi ya vijana 300,000 wanabaki. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuanzisha kambi maalum ili kusudi sasa vijana hawa waweze kupata misaada ya kutosha ya utaalam wa kilimo na ufugaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu; leo jioni usifanye mazoezi, umeshafanya ya kutosha hapa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo ni zuri, hata hivyo Serikali imesha-*take initiatives* za kutosha katika eneo hilo, ndiyo maana Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali, na hivi sasa mikoa mbalimbali wameshaanzisha kambi za vijana katika jitihada za kujenga ujasiriamali, ujasiri na uzalendo. Jambo hilo limetokea katika Mkoa wa Tabora pamoja na Pwani na mikoa mingine na zoezi hilo linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tuwashukuru wenzetu wa taasisi binafsi hasa shirika la *Plan International* ambalo kupitia mikoa mbalimbali kama vile Mkoa wa Morogoro, Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Pwani na mikoa mingine wameanza kupitisha programu maalum ya vijana kwa ajili ya kuwawezesha katika fani mbalimbali za ufundi. Hili limetoa mafanikio makubwa, zaidi ya vijana 9,500 wamepata *skills* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba Serikali itawatumia wadau mbalimbali na nguvu za Serikali lakini na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya nawashukuru sana, wameshaanza ku-*take* hiyo *initiative* kwa kufanya mabadiliko hayo makubwa; naamini tukifanya hivi tutawasaidia sana vijana wetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso, ajiandae Mheshimiwa Raymond.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri zilizo nyingi zinashindwa kutenga hii asilimia kumi kwenye Mfuko wa Vijana na Wanawake na hii inathibitishwa na ripoti mbalimbali za *CAG*, na ni ukweli kwamba tuna Mifuko karibu 19 ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Je, Serikali haioni sasa iko haja ya kupunguza Mifuko hii angalau kati ya miwili mpaka mitano ikiwemo hii iunganishwe kuwe Mfuko mmoja ili kuwe na ufanisi na iwafikie kweli wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ku-*harmonize* hii Mifuko tuwe na Mfuko mmoja nadhani ni suala la kuzungumzika, tutafanya tathmini ya kina. Hata hivyo katika Mfuko wa asilimia kumi kuna maelekezo sasa hivi tunayatoa. Sasa hivi zile fedha katika *ten percent* zinaingia katika *deposit account* kama unaingiza katika *dust bin* mwishowe hata *assessment* hatuwezi kufanya vizuri; ndiyo maana sasa hivi tunaangalia jinsi gani tutafanya; kama ikiwezekana tuwe na akaunti maalum ya Mfuko katika Halmashauri ili tuweze kui-*monitor* vizuri; ili zikiingia zinazorudi kutoka kwa watakaokopa tuweze kuisimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wazo zuri tutaendelea kuchukua yote haya ili hatimaye tuboreshe Mifuko hii iweze kuwasaidia vijana na akinamama na hatimaye tutatengeneza ajira kwa wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa uwezo wa Halmashauri unatofautiana na Halmashauri nyingine ni duni kabisa hazina kipato zikiwepo Halmashauri za Hai, Siha, Rombo na kwingineko; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kufanya *top up* ili nia yao njema ya kuwezesha wanawake na vijana ifanane Tanzania nzima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la mama ni zuri, Halmashauri zingine pato lake ni dogo lakini kutokana na wazo hilo zuri ndiyo maana Serikali ina mifuko mingine ya ku-*top up.* Kuna Mfuko kutoka katika *empowerment* programu yetu ambayo inasaidia na tuna fedha nyingi sana hapa, takribani kuna Mifuko 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni wazo zuri lakini Serikali imeshachukua *initiative* tayari, Mifuko hiyo ipo, isipokuwa jamii yetu wakati mwingine hawana taarifa sahihi kuhusu mifuko hiyo. Ndiyo maana sasa wakati programu hii inaendeshwa hapa Dodoma takribani mwezi mmoja uliopita uwezeshaji huo umeshatolewa na tumewaelekeza sasa Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii waweze kushuka katika *grassroot* ili kuweza kuwaelimisha wananchi ni wapi watapata hizi fedha na uwezeshaji ili kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wazo zuri na Serikali hivi sasa inaendelea ku-*top up* isipokuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wafanye kazi yao sasa kuhakikisha jamii sasa inapata uelewa wa kutosha juu ya mifuko hii ili waweze kupata uwezeshaji wa kutosha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Kigola.

Na. 429

**Ujenzi wa Vituo vya Afya vya Kata za Mninga na Mtwango**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Mninga na Mtwango bado haujakamilika, hivyo wananchi wa Kata hizo wanaendelea kupata shida ya matibabu:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa vituo hivyo ili wananchi waweze kupata huduma za matibabu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mtwango ulianza mwaka 2012, ambapo umeshagharimu Sh.22,500,000/=. Aidha, Kituo cha Afya Mninga kilianza kujengwa mwaka 2008 ambapo umegharimu Sh.41,000,000/=. Vituo hivyo vipo katika hatua ya umaliziaji wa majengo ya *OPD* na nyumba za watumishi ili huduma zianze kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Serikali ilitenga Sh.32,500,000 kwa ajili ya kuendelea kuchangia ukamilishaji wa Vituo vya Afya Kata ya Mninga na Mtwango. Fedha zilizopokelewa mpaka sasa ni Sh.8,000,000/=. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, zimetengwa Sh.65,000,000/= kwa ajili ya kuimarisha Vituo vya Kasanga na Kituo cha Afya Mbalamaziwa katika Jimbo la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mpango wa Serikali kuunga mkono juhudi za wananchi katika miradi ya maendeleo kwa kutenga fedha kupitia *LGDG* kila mwaka ili kumalizia miradi mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri. Hivi vituo vilianza miaka mingi sana, sasa hivi ni miaka tisa bado havijakamilika na mimi swali langu nimesema ni lini sasa Serikali itamaliza ujenzi huu kwa sababu umechukua muda mrefu sana? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesema itapeleka Sh.35,500,000 na imeshapeleka Sh.8,000,000 tu, bado Sh.24,000,000 bado. Je, ni lini Serikali sasa itapeleka hii fedha Sh.24,000,000 ili ujenzi ule ukamilike? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, tulipokuwa kule *site;* miongoni mwa maeneo tuliyotembelea ni Sekta ya Afya katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli hivi sasa imepelekwa shilingi milioni nane, bado takriban shilingi milioni 24. Hata hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge; hivi leo asubuhi nilikuwa naongea na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Bwana Shemdoe. Katika mambo ambayo tumekubaliana ni kwamba atenge fedha kwa kadri inavyowezekana kuhakikisha vituo hivi vinakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wazi kwamba Jimbo la Mufindi Kusini ni miongoni mwa Halmashauri tajiri ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rasilimali walizonazo zikisimamiwa vizuri tutaweza kufanya vitu vingi zaidi. Kwa hili Mkurugenzi amenipa *commitment* leo hii asubuhi wakati naingia getini, amesema kwamba atashirikiana na Waheshimiwa Wabunge ahakikishe miradi yote ambayo bado haijakamilika watumie fedha, *own source,* wakamilishe miradi yote wasiwe na viporo tena vinavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itasimamia vizuri, lakini kwa sababu na wao wamejipanga vizuri, yeye na Mheshimiwa Mgimwa, nadhani hakuna kitu kitakachoharibika katika Halmashauri yao kwa sababu ni miongoni mwa Halmashauri tajiri, *own source* yao ni kubwa kuliko jambo lingine lolote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Bilakwate na Mheshimiwa Bilago.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Nami naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Hospitali ya Mji wa Mafinga inahudumia Halmashauri mbili za Wilaya ya Mufindi na Mji wa Mafinga. Hata hivyo, katika fedha za *Basket Fund,* Halmashauri ya Mji

wa Mafinga inapokea kiasi kidogo kiasi kwamba inaathiri utendaji wa Hospitali ya Mafinga ambayo inahudumia Halmashauri zote mbili. Je, ni lini Serikali itaongeza fedha za *Basket Fund* kwa ajili ya Hospitali ya Mji wa Mafinga ambayo inahudumia halmashauri zote mbili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Chumi, siyo jambo la uongo. Ni kweli Halmashauri ya Mafinga pale ukiangalia ule Mji, wananchi wa Mufindi wote wanakuja kutibiwa pale Mafinga. Bahati mbaya ukifanya *comparison;* ulinganifu wa *Basket Fund* ya Mafinga na Mufindi, Mafinga *Basket Fund* yao ni ndogo, lakini wagonjwa wote wanakuja kutibiwa Mafinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *scenario* hiyo iko sambamba na kule Tarime, Halmashauri ya Mji wa Tarime na Halmashauri ya Tarime nanii, kwamba ya Mji ina fedha kidogo, lakini Halmashauri hii ina fedha nyingi lakini ha-*top up* nanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, maeneo ambayo Halmashauri haina Hospitali ya Wilaya lakini kuna hospitali mfano ya Taasisi ya Dini, wanatumia kituo kile kama *DDH* na wanapeleka fedha. Sasa tujiulize, kama watu wa Mufindi hawana hospitali, wanatumia Hospitali ya Mafinga na kama wangekuwa hawana Mafinga, maana yake kungekuwa na hospitali ya *private* pale ya *DDH,* wangeitumia kama hivyo na kupeleka fedha. Kwa nini hapa msikae sasa kufanya *harmonization* ya jambo hilo kulifanya liwe vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuseme kwamba jambo hili tumelichukua na nitalikabidhi katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tutaangalia nini tufanye. Lengo kubwa ni kwamba mwisho wa siku, Halmashauri ya Mafinga na Hospitali ya Mafinga iweze kujiendesha vizuri kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bilakwate, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Joyce na Mheshimiwa Ryoba Chacha, wajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kama lilivyo swali la msingi, kwenye Jimbo langu la Kyerwa, wananchi wameanzisha vituo ambavyo wameshaanza ujenzi, wamefika kwenye kumalizia boma. Kwa mfano, kama Kata yangu ya Kimuri, kuna wananchi ambao wamejenga boma limefikia kwenye lenta na wameweza kujenga maboma zaidi ya kumi. Maboma haya yamekaa karibu miaka saba. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha maboma haya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nikupe taarifa, Mheshimiwa Bilakwate anapoishi kwake pale wakati mwingine ninapofika pale hata mtandao wa simu anapata nchi ya Rwanda. Bahati mbaya hana Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya suala hili la maboma, kutokana na ombi lake tumeamua kujenga *theater* sasa na sehemu ya kupasulia wagonjwa pamoja na kupata huduma nyingine katika Kituo chake cha Afya cha Mulongo. Tumefanya hivi ili eneo lake liweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumefanya *assessment* ya maboma yote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jinsi gani tutayamalizia, yale ya Vituo vya Afya na Zahanati, takriban shilingi bilioni 950 zinahitajika. Katika mwaka huu wa bajeti tumeshatenga karibu shilingi bilioni takriban 95. Lengo kubwa ni kuhakikisha tunamalizia hivi viporo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Local Government Capital Development Grant,* tumetenga karibu shilingi bilioni 251, karibu *one third* ya fedha hizo zinakwenda katika suala zima la umaliziaji wa maboma. Kwa hiyo, nawaagiza Wakurugenzi wote wakiwemo na wa Halmashauri yake; inapofika ile fedha, naomba tuweke mgawanyo mzuri wa jinsi gani tutakavyomalizia maboma haya na siyo ya afya peke yake, hata katika Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto na wale niliowataja naomba mjiandae.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na Serikali kufanya jitihada kubwa katika kuhimiza ujenzi wa Vituo vya Afya, kumetokea tatizo kubwa sasa hivi ambalo linakabili vituo ambavyo vimekwisha; ni upungufu wa watoa dawa za usingizi. Kwa hiyo, nataka nijue tu, kwa kuwa Vituo vya Afya vingi vitajengwa katika nchi yetu, Serikali imejipangaje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana. Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mwamoto kwa swali lake zuri. Ni kweli tunategemea mpaka mwisho wa mwezi Desemba, takriban Vituo vya Afya 100 vitaweza kufanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni. Kwa hiyo, tayari tumeshaongea na Chuo Kikuu cha *KCMC* kwa ajili ya kuendelea kutoa kozi mahususi za wataalam wa usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muda huu pia, wale ambao wako tayari katika maeneo ya kazi, tumeandaa mpango wa kuweza kupewa mafunzo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tahadhari, wataalam wangu wanasema tusifanye mafunzo ya haraka, matokeo

yake badala ya kuwaokoa akinamama wajawazito tukawaua. Kwa hiyo, tuna-*negotiate* muda wa mafunzo haya uwe angalau miezi 9 au 12. Wataalam wamekataa muda usiwe chini ya miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo suala tunalifanyia kazi na naamini Mheshimiwa Waziri wa Utumishi yuko hapa, kwa hiyo, pia atatusaidia katika kuajiri wataalam hawa wa usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joyce, atafuatiwa na Mheshimiwa Chacha na Mheshimiwa Bilago .

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, mapema mwaka huu alifanya ziara katika Mkoa wa Arusha hususan katika Jimbo la Monduli na akatembelea Vituo vya Afya vya Makuyuni na Kigongoni. Vituo hivyo vilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi na kufikia kwenye lenta na aliahidi kuvimalizia mapema mwaka huu au mwaka kesho. Naomba maoni ya Mheshimiwa Waziri, je, ni lini atatoa fedha hizo za kumalizia Vituo hivyo vya Afya vya Jimbo la Monduli? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mjibu kwa kifupi. Muda wetu unakwenda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli siku ile nilifika Arusha, nikafika Monduli na *priority* yetu ni kwamba tumeitenga pale na *commitment* tuliyoifanya ni kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mto wa Mbu ambapo tumezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimewapongeza wananchi kwa juhudi kubwa wanayoifanya katika suala zima la ujenzi wa Vituo vya Afya. Kwa hiyo, ni

*commitment* ya Serikali na tuko katika michakato ya aina mbalimbali, tutaweza kukamilisha mambo haya kwa kadri inavyowezekana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ryoba, halafu Mheshimiwa Bilago.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Jimbo la Serengeti, Vituo vya Afya vya Iramba na Nata vimetengewa fedha kwenye mwaka huu wa bajeti pamoja na Hospitali ya Wilaya ambayo imetengewa shilingi milioni 700. Leo ni tarehe 21, tarehe 30 mwaka wa fedha huu tulionao unaisha; na Mheshimiwa Waziri alipokuja pale Jimbo la Serengeti, alituhakikishia kwamba fedha zitakuja. Nini tamko lake kuhusu fedha hizi kutokufika mpaka sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilikuwa na Mheshimiwa Ryoba Jimboni kwake na tulitembelea ile Hospitali ya Wilaya, nami nilikuwa najua kwamba jana ndiyo angeunga mkono Bajeti ya Serikali kwa sababu ndiyo fedha zenyewe hizi zinazopelekwa kwa wananchi. Sasa tunapokuja *site* pale tunakubaliana fedha ziweze kwenda, tunapokuja huku katika kupitisha mafungu wenzetu mnasusa hamtaki kupitisha, sio jambo zuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ryoba, tumekwenda pale tumeona matatizo ya wananchi. Sawa! Suala la fedha tutakwenda kulitekeleza na kama tulivyoongea kwa kirefu zaidi, pale ukiangalia kupitia Ofisi yetu na Wizara ya Afya katika lile jengo la pale Mugumu tunafanya ile *two in one sword,* tutafanya lile na wananchi watapata huduma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Buyungu, Wilaya ya Kakonko tumepata ufadhili wa kujengewa vituo vya kisasa vya baba, mama na mtoto kutoka Bloomberg, *USA.* Ni vituo vya kisasa kabisa. Sasa nataka *commitment* ya Serikali, vituo vile vinawekewa vifaa vya kisasa na vinahitaji wataalam wa kisasa. Je, Serikali iko tayari kuleta wataalam baada ya vituo hivyo kukamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Kakonko ni eneo ambalo linapata changamoto kubwa sana. Ndiyo maana siku ile nilivyokuwa naongea na watumishi wetu pale Kakonko mpaka kama binadamu unajisikia huzuni kwa *cost load* waliyokuwa nayo, ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie, kwa sababu Serikali ipo katika mpango wa kuajiri watumishi wengi; na najua katika Mkoa wa Kigoma tumepeleka watumishi wapatao takribani tisa au 12, kati ya hapo tu kwa Mkoa mzima wa Kigoma, lakini mahitaji ni makubwa zaidi. Ngoja mchakato huu sasa wa ajira hizi mpya utakapotoka tutaangalia jinsi gani tusaidie wananchi wa Kakonko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siyo kwa Kakonko peke yake na Mkoa wa Kigoma wote kwa ujumla kwa sababu kuna changamoto kubwa ya wakimbizi, kwa hiyo, huduma inakuwa ni *tight* sana. Kwa hiyo, lazima tutalichukua jambo hilo; Kasulu, Kakonko, Kibondo, Uvinza na sehemu nyingine, kutoa kipaumbele kwa Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Dkt. Sware.

Na. 430

**Tathmini ya Misitu ya Asili**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Idara ya Misitu ina jukumu la kutathmini rasilimali zake ikiwemo miti:-

(a) Je, Wizara inatekeleza kwa kiwango gani katika kufanya tathmini za idara zake kuangalia athari za magonjwa ya miti?

(b) Je, nchi inazo ekari ngapi za mioto ya asili na iliyopandwa?

(c) Je, hadi sasa ni ekari ngapi za miti zimekatwa kwa ajili ya mbao na mkaa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002, shughuli zote za utafiti za kitaalam kuhusiana na magonjwa ya miti na athari zake hutekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Misitu *(TAFORI)* chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Taasisi hii hufanya utafiti wa utambuzi wa aina ya magonjwa, ukubwa wa matatizo na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua kutegemeana na uzito wa matokeo ya utafiti husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Tathmini ya Rasilimali Misitu *(NAFORMA)* iliyotolewa mwaka 2015 inaonesha kuwa nchi yetu ina misitu yenye hekta milioni 48.1

ambapo misitu ya asili ni hekta 47.528, sawa na asilimia 98.8 na misitu ya kupandwa ni hekta 572,000, sawa na asilimia 1.2 tu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kasi ya uharibifu wa misitu ni kubwa sana bila kujali aina ya uharibifu wa misitu ambapo kiasi cha ekari 372,000 za misitu huangamizwa kila mwaka nchini. Aidha, takwimu zinaonesha kwamba ili kurejesha hali ya misitu nchini katika viwango vyake vya kawaida, kiasi cha jumla ya ekari 185,000, sawa na jumla ya miti milioni 230 kinahitajika kupandwa kila mwaka kwa kipindi cha miaka 17.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa tunajua umuhimu wa misitu na miti na kazi zake katika jamii na katika ekolojia, ni vizuri tukajua kwamba afya ya miti au misitu yetu ikoje. Sasa kwa kuwa kuna changamoto ya kibajeti kwenye Idara hizi za Tafiti za Misitu, napenda kujua Wizara inajipangaje ili kuweza kuweka sawa tathmini ya hali ya misitu nchini *in terms* za afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kujua kwamba, Wizara inaweka mikakati gani madhubuti ili kuweza kuondokana na changamoto ya upotevu wa misitu kutokana na kukata miti ovyo au uvunaji holela wa miti? Sasa Serikali inajipangaje kujua ni aina gani ya miti na idadi ya miti inapangwa sehemu gani na inashirikishaje jamii ili zoezi hili liwe na manufaa na endelevu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza, Wizara imejipangaje katika kuangalia afya ya miti? Kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, chini ya Taasisi ya *TAFORI* ambayo ni mahususi

kabisa kwa ajili ya kufanya tafiti, Serikali inafuatilia hali ya misitu nchini kwa namna ambayo ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wote tunaangalia misitu yetu inaendaje ili kuweza kubaini matatizo yanayoweza kutishia uharibifu wa misitu kutokana na magonjwa na changamoto nyingine zinazohusiana na afya ya miti kwa mfululizo ambao, kwa kuwa ni endelevu, changamoto zinazoonekana zinashughulikiwa mara tu zinapogundulika huko kwenye misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawezekana kupitia jitihada mbalimbali ambazo ni za Serikali kwa maana ya kupitia bajeti za ndani. Pia kwa sababu suala la uharibifu wa mazingira, masuala ya maendeleo endelevu; haya ni masuala yanayotazamwa na dunia nzima kwa pamoja kwa sababu uharibifu wa mazingira unaathiri dunia yote kwa pamoja. Kwa hiyo, kupitia taasisi mbalimbali ambazo zina maslahi katika kuhakikisha kwamba kuna maendeleo endelevu na utunzaji wa misitu unakuwepo, Taasisi hii ya *TAFORI* mara kwa mara kwa kupitia maombi mbalimbali inapata *support* ya kibajeti na kuweza kukamilisha majukumu hayo.

Meshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, napenda kusema kwamba tunao Mkakati wa Taifa wa Kupanda na Kutunza Miti. Hapo awali tumekuwa tukielekeza nguvu kwenye kupanda miti peke yake, lakini sasa baada ya kuona kwamba baada ya kupanda miti bila kufuatilia utunzaji wake na kuhakikisha kwamba inakua, tunapoteza asilimia kubwa sana ya miti ambayo tumetumia rasilimali nyingi sana katika kuipanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mkakati huu wa Taifa wa sasa hivi unaopita katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kuanzia mwaka 2016 mpaka mwaka 2020, Ofisi ya Makamu wa Rais ikiwa ndiyo inayoongoza, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo pamoja na Sekta Binafsi, wote katika mkakati huu wamegawana majukumu ya kuhakikisha

kwamba tunafanya jitihada za kufikia lengo hili ambalo nimelisema hapo awali la kuweza kufikia upandaji wa miti 1,075,000 kila mwaka katika muda wa miaka 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya muda mfupi misitu yetu itakuwa katika hali yake ya afya ya kawaida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi, halafu Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa nia ya Serikali ni kupanda miti nchi nzima ili kurudisha uoto wa asili uliopotea na vikundi vya Wilaya ya Lushoto vimeanza kutosha miche ya miti, hasa Kikundi cha *Friends of Usambara.* Je, Serikali itasaidiaje vikundi hivi, hasa hiki cha *Friends of Usambara,* maana mpaka sasa kimeshaotesha miche zaidi ya milioni tatu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali inaunga mkono jitihada zote ambazo zinafanywa na mtu mmoja mmoja, lakini pia hata na vikundi. Hii ni taarifa njema ambayo Serikali inapokea kwa mikono miwili, uwepo wa vikundi katika eneo ambalo amelizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba awaelekeze wale wanakikundi waweze kuwasiliana na Wizara ili tuweze kuona namna gani Wizara inaweza kuwa-*support.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ina misitu mikubwa miwili; kuna ule msitu ambao unahifadhiliwa na *WMA* (Ustawi wa

Vijiji) na ule msitu wa Serikali ambao ni Msitu wa Nyera, Kipelele. Msitu huu ni msitu ambao tumeurithi kutoka enzi za Wakoloni, lakini mpaka leo *harversting plan* ya msitu ule haijatoka. Nini kauli ya Serikali kuharakisha *harvesting plan* ya msitu huu ili wananchi waweze kupata faida ya kuwepo kwa msitu huu wa Nyera, Kipelele? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika misitu miwili anayoizungumzia, labda niseme tu kwa ujumla, *harvesting plan* anayoizungumzia maana yake ni mpango wa uvunaji. Tunao mpango wa uvunaji ambao tumeupitisha hivi karibuni unaoeleza namna ambavyo tunaweza tukavuna misitu lakini tukizingatia uvunaji endelevu ili uvunaji usizidi kasi ya kukua kwa misitu na hatimaye tukajikuta kwamba tunamaliza misitu zaidi ya kuitunza na kuifanya iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati wowote ule Mheshimiwa Mbunge atakapopata nafasi aje Wizarani, tunaweza tukamwelekeza namna gani au tunaweza tukamwonesha *harvesting plan* jinsi ilivyo aweze ku-*share* na wananchi wa maeneo ambayo yanahusika kwa ajili ya matumizi ya wananchi wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata ambalo ni la Mheshimiwa Kaboyoka.

Na. 431

**Msitu wa Shengena Wilayani Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Sehemu kubwa ya Misitu ya Hifadhi ndani ya Wilaya ya Same ni Msitu wa Shengena ambao ni chanzo cha Mito mikubwa ya Nakombo, Hingilili, Yongoma na Saseni ambayo

maji yake yanatumiwa na wakazi wa Majimbo ya Same Mashariki, Mlalo na Korogwe Vijijini:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha doria kulinda Msitu wa Shengena kuzuia uharibifu unaoendelea ikiwemo uchomaji moto ambao pia unaathiri maisha ya watu?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha utaratibu wa uvunaji wa miti iliyokomaa katika Msitu wa Shengena na kuweka mkakati wa kuotesha miti mingine ili msitu uwe endelevu?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya athari za kimazingira zinazotokana na uchimbaji wa madini ya *Bauxite* unaoendelea katika Msitu wa Shengena?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali ya Wilaya ya Same imekuwa ikitekeleza shughuli za doria na *operations* za mara kwa mara katika hifadhi za misitu ambapo wahalifu wanaopatikana na hatia ikiwa ni pamoja na uchomaji moto huchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuwa uharibifu wa misitu unahusisha baadhi ya wananchi wasiozingatia Sheria, Serikali inakamilisha mpango wa usimamizi shirikishi na wananchi wa vijiji vyote 23 alivyovitaja vinavyopakana na hifadhi ya Chome ushiriki ambao utaboresha ulinzi wa hifadhi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa misitu ya mazingira asilia pamoja na mambo mengine unazingatia kutokuvuna miti hata baada ya kukomaa na pia kuacha miti ya asili iendelee kuota yenyewe badala ya kupanda miti

mingine ili kulinda hifadhi na kuendeleza mfumo wa kiikolojia na bioanuwai zilizopo ndani ya hifadhi. Aidha, hatua hii inalenga kutunza, kuhifadhi na kuendeleza mfumo wa ikolojia ikiwa ni pamoja na vyombo vya maji na viumbe hai waliopo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa madini katika maeneo ya hifadhi husimamiwa na sheria zikiwemo Sheria za Madini ya mwaka 2010, Sheria ya Misitu namba 14 ya mwaka 2002 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira *(NEMA)* ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hakuna taarifa rasmi zinazohusu uchimbaji wa madini ya *Bauxite* katika Hifadhi ya Msitu wa Shengena. Aidha, iwapo mtu yoyote binafsi au taasisi itahitaji kufanya shughuli za uchimbaji madini ndani ya hifadhi hiyo, atatakiwa kufuata taratibu za kisheria zitakazozingatia masuala yote muhimu ikiwemo kufanyika kwa tathmini ya athari ya mazingira kabla ya kuanza kwa uchimbaji huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, uvunaji wa miti hata baada ya kukomaa unakatazwa; na kwa kuwa Jimbo la Same Mashariki hakuna hata vitalu vya miti. Je, ni namna gani Serikali itahakikisha kwamba kunaanzishwa vitalu ili wananchi waweze kupata miche ya kuweza kupanda kwenye maeneo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wengi walihamasishwa na walipanda miti mingi na wengi walichukua mikopo ili wapande miti kwa biashara, lakini inapofika wakati wa uvunaji wanahangaishwa sana na Halmashauri hata pale Wizara ilipotoa maagizo kwamba waruhusiwe kuuza miti yao. Je, Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani hasa kwa Halmashauri ya Same ili wajue kwamba

Wizara ina msimamo gani juu ya suala la wananchi waliopanda miti yao waweze kuivuna na kuiuza kibiashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kaboyoka katika swali lake la kwanza, anataka kujua ni namna gani Serikali itawawezesha wananchi wa kule Same Mashariki kuwa na vitalu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali lililotangulia, katika mkakati wa upandaji miti Kitaifa, kila Halmashauri ya Wilaya imepangiwa kupanda miti kwa wastani wa miti milioni mbili kila mwaka. Nasema ni wastani, kwa sababu itazingatia ukubwa wa Halmashauri, idadi ya watu, hali ya hewa ya Halmashauri inayohusika, kuona maeneo rafiki ambayo miti inaweza kupandwa. Kwa hiyo, ziko Halmashauri nyingine zitapanda miti zaidi ya hiyo, Halmashauri nyingine zinaweza zikapanda miti pungufu ya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uwepo wa vitalu vya miti ni suala ambalo litafanyika baada ya kazi ya mkakati huu kuwa imefikia katika Halmashauri hiyo na kwa hiyo, mtaweza kupata ushauri kutoka Wizarani chini ya mkakati huo nilioutaja ili muweze kuoneshwa ni maeneo yapi, ya ukubwa gani muweze kuwa na vitalu vya kuweza kupanda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili la Mheshimiwa Kaboyoka, anataka tamko kuhusiana na miti ambayo inakatwa kwenye maeneo ambayo ni ya miti ya kupandwa ukilinganisha na hatua za udhibiti kwa mujibu wa sheria ambayo inazuia ukataji miti hovyo ambayo inaendana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba ni jukumu la Serikali sasa

kuweza ku-*balance* na tunaposimamia ukataji wa miti kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo mkaa na matumizi mengine, hatutakataza matumizi ya miti halali ambayo imepandwa kwa njia halali, isipokuwa usimamizi wake unaendana na upataji wa vibali mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Taasisi chini ya Wizara zilizoko katika Halmashauri hiyo zitaweza kutoa utaratibu ambao chini ya utaratibu huo miti halali iliyopandwa kwa madhumuni hayo ikiwa imekidhi vigezo vya kisayansi kama vile kukomaa na mambo mengine, utaratibu huo hauwezi kuzuiliwa.

Mheshimiwa Mbunge, ufafanuzi zaidi kuhusiana na suala hili unaweza ukapatikana wakati wowote ule baada ya *session* hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf, halafu Mheshimiwa Shangazi atafuata.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ni dhahiri mbinu zote za ulinzi zinazotumika pamoja na ulinzi shirikishi bado hazijasaidia kutatua tatizo la uharibifu wa misitu na hususan misitu ya asili kwenye nchi yetu. Je, Serikali inafikiria nini sasa kuhusu mbinu mbadala ya kuhakikisha kwamba misitu yetu inahifadhiwa na kuendelezwa kwa ajili ya kizazi kijacho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana, muda wetu umekwenda. Leo tumeawaachia Waheshimiwa Wabunge mwonyeshe uwezo wenu na utaalam wenu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siyo jambo jema sana kuthibitisha hapa kwamba jitihada zote zile za kisheria na zile za kupitia ushirikishaji wa wananchi zimeshindikana kuweza kuzuia tatizo hili la uharibifu wa mazingira. Napenda kuungana na Mheshimiwa Mbunge kuona kwamba jitihada hizo bado zipo

na zinatakiwa kuendelea. Tunatakiwa tu kuboresha namna ambayo tumekuwa tukifanya hapo nyuma, maisha bado yanaendelea ili tuweze kuhakikisha kwamba uhifadhi wa mazingira unaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaongeza idadi ya Wataalam ili waweze kusimamia vizuri zaidi, lakini pia tutaweza kusimamia misitu ili tuweze kupunguza uharibifu wa mazingira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, wajiandae Mheshimiwa Mulugo na Mheshimiwa Zakaria Issaay.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa uwepo wa Msitu wa Shengena, Msitu wa *Shangai* na Msitu wa Bombo ndiyo unaosaidia uwepo wa Hifadhi ya Mkomazi; lakini katika Msitu huo wa Bombo kuna uvamizi mkubwa unaofanywa na wananchi. Je, ni lini sasa Serikali itaweka mipaka *(beacons)* kutenga eneo hili la Msitu wa Bombo ambao ni msitu maalum wa kuvuta mvua? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kabisa msitu wa Bombo ni msitu muhimu sana kwa ajili ya Hifadhi ya Mkomazi, lakini pia kwa ajili ya ikolojia nzima ya eneo la Mkomazi. Sasa lini Serikali itaweka *beacons?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la uwekaji wa *beacons* linaendelea nchi nzima na nataka nimhakikishie kwamba kama bado hatujafika Mkomazi, nitakwenda kuangalia ratiba na kuona lini tunafika huko ili niweze kumpa tarehe kabisa, lini tunaweka katika hifadhi hiyo. Kwa hiyo, tuonane baada ya hapa, tuweze kuona ni lini *beacons* zinawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni mpango wa Serikali ambao unaendelea sasa hivi kuweka *beacons* au kuweka alama za mipaka katika hifadhi zote nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo, ajiandae Mheshimiwa Zakaria Issaay.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kuweza kupata muda wa kuuliza swali moja la nyongeza. Mamlaka ya Wanyamapori maeneo ya Ngwala, Itiziro na kule Guwa wamevamia vijiji hivyo na hivyo wamewasambaza wananchi, wamewanyang'anya mashamba, wamenyang'anya mbao na mali zao nyingine; na Mheshimiwa Naibu Waziri nilikwambia. Sasa nataka Mheshimiwa Naibu Waziri anithibitishie humu ndani mbele ya Bunge kwamba ni lini tutaongozana mimi na yeye twende tuka-*solve* mgogoro huo kwa ajili ya wanyamapori maeneo ya Ngwala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi kama ulivyoelekeza, ni kwamba kwanza mpaka unahusisha pande mbili na ni vigumu sana upande mmoja kusema mwingine amemwingilia mwingine kwenye mpaka wake. Nafikiri njia sahihi, wote wawili wanaweza wakawa mahali pamoja halafu kila mmoja akaangalia vigezo nani ameingia kwa mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake, lini tutaweza kwenda; nilimwambia kabla na narudia tena kusisitiza, tukimaliza Bunge hili la Bajeti mimi na yeye tutapanga ratiba ambayo itakuwa ni rafiki, twende kwenye maeneo hayo, halafu tutaangalie namna gani tunaweza kutatua tatizo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo la Mbulu Mjini mipaka yake kwa asilimia 50 inazungukwa na misitu ya asili na maji wanayotumia viumbe wakiwemo binadamu yanatoka katika misitu hiyo. Hivi sasa maji hayo yameanza kupungua ndani ya misitu. Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam watakaofanya utafiti katika

misitu inayozunguka Jimbo la Mbulu Mjini ili iweze kufanyia kazi taarifa yake ya utafiti kwa ajili ya kushauri jamii inayozunguka misitu hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, anataka kujua ni lini tu!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kusema tu Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba ameshafika Ofisini kwangu siyo mara moja na suala hili tumelizungumza, tumeliweka wazi, tumesema kwamba nina maslahi kwa wananchi wa Jimbo lile. Kwa hiyo, ni lini tunaenda? Jibu ni lile lile ambalo nilisema kabla; nimemwambia Ofisini na narudia tena hapa kwamba mara baada ya Bunge hili la bajeti, nina ziara ndefu sana, ratiba hiyo inahusisha pia Jimbo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya. Mheshimiwa Juma Othman Hija.

Na. 432

**Tofauti ya Virusi vya UKIMWI na Ugonjwa wa UKIMWI**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Wataalam wa Afya wanaeleza kuwa mtu anaweza kuwa na virusi vya UKIMWI lakini hana ugonjwa wa UKIMWI:-

Je, nini maana ya maelezo haya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Jimbo la Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mtu anaweza kuwa na virusi vya UKIMWI lakini hana ugonjwa wa UKIMWI. Maana yake ni kuwa, mtu atakuwa na ugonjwa wa UKIMWI pale ambapo kinga zake zinapokuwa zimeshuka sana na hivyo kuanza kupata magonjwa nyemelezi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha kuwa na virusi vya UKIMWI bila kuonyesha dalili za ugonjwa wa UKIMWI kawaida kinaweza kuchukua muda mrefu kuanzia miaka mitano hadi kumi zaidi tangu mtu apate maambukizi ya virusi vya UKIMWI. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hija.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tafsiri hii ni nzuri sana, lakini ni ya kitaalam zaidi. Je, sasa Serikali ina mpango gani kuwaelimisha wananchi juu ya tafsiri hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimhakikishie tu Mheshimiwa Hija kwamba toka maambukizi ya virusi vya UKIMWI yalipotokea miaka ya mwanzo ya 1980 Serikali pamoja na wadau mbalimbali tumekuwa tukishirikiana kuelimisha wananchi juu ya virusi vya UKIMWI, UKIMWI, magonjwa nyemelezi, lakini pia madhara yanayotokana na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hiyo imeendelea na imefanyika kwa ufanisi mkubwa na kwa mafanikio makubwa sana. Ndiyo maana leo hii ninavyozungumza hapa, kiwango cha maambukizi ya UKIMWI kimepungua sana mpaka kufikia sasa hivi tuna kiwango kama cha asilimia 4.6 tu *(prevalence rate).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo tuna mafanikio makubwa sana kwenye eneo hili kuliko

anavyofikiria. Vile vile tutaendelea kutumia mbinu ambazo tumekuwa tukitumia, lakini pia ubunifu wa taasisi mbalimbali tunazoshirikiana nazo kuweza kuzidisha uelewa wa wananchi juu ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa ufupi nitoe elimu tu kidogo hapa kwamba virusi vya UKIMWI, yaani VVU ama *HIV* ama kitaalam *Human Immunal Deficiency Virus,* ni kirusi ambacho kipo katika familia ya *retroviridae* na viko virusi vingi vinavyosababisha magonjwa mbalimbali yanayosababishwa na virusi hiki nacho kimo katika kundi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kinayofanya ni kuingia kwenye chembe chembe ya mwanadamu ya aina ya *white blood cell* ambayo inahusika na kinga mwilini na kitakaa mle kwa miaka kati ya hiyo mitano mpaka 10 hadi 12 bila kujulikana na baada ya hapo sasa kama mtu alipima atajulikana, lakini kama hakupima, haitajulikana kwamba ana maambukizi. Kuanzia hapo zile *cells* za kinga zitapungua mwilini na mtu sasa ataanza kuonesha dalili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale mtu anapoanza kuonesha dalili kwamba amepungua kinga mwilini, ndiyo tunasema amepata UKIMWI. Hiyo ndiyo tofauti. Isipokuwa unaweza ukaishi na hicho kirusi kwa muda huo niliousema bila kuonesha dalili; na kwa maana hiyo, utakuwa na kirusi tu, lakini hauna UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa UKIMWI maana yake ni ugonjwa unaokuja baada ya kuwa umeambukizwa virusi vya UKIMWI labda miaka mitano ama kumi huko nyuma, kinga ikashuka, sasa ndiyo unaanza kupata UKIMWI na kwa sababu kinga imeshuka, magonjwa ambayo kwa kawaida hayatokei kwenye watu wenye afya, yanaanza kutokea kwako kama magonjwa mbalimbali ya *cancer* mbalimbali, kama *Kaposi's sarcoma*, magonjwa ya kukohoa kama Kifua Kikuu, magonjwa ya kifua kisichopona mara kwa mara; magonjwa ya ngozi kama *herpes zoster* na vitu vingine. Kwa hiyo, hapo tunasema sasa una UKIMWI.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lyimo, wajiandae Mheshimiwa Khadija, Mheshimiwa Mgeni na Mheshimiwa Fredy.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wote tunajua kwamba maambukizi ya virusi vya UKIMWI au UKIMWI yanatokana na sababu kubwa ya kuwa na *sexual partners* wengi; lakini kwa hapa Tanzania na duniani kote inaonekana wanawake ndio wanakuwa wengi kuliko wanaume. Je, Mheshimiwa Waziri anatuambia sababu hasa ni nini? Kwa nini wanawake wanakuwa na maambukizi kuliko wanaume? Je, tatizo ni kwamba wanaume ndio wanawaambukiza zaidi au wanawake wanakosa maadili? Tusaidie kwa hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wewe ni mtaalam, lakini tunaomba majibu kwa kifupi sana, muda wetu umekwisha. Nimetoa tu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nitazingatia muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba wanawake wanaambukizwa zaidi kuliko wanaume; uwiano hauko mbali sana, tofauti ni ndogo, lakini ni kweli kwamba maumbile ya kibaiolojia ya wanawake ni tofauti sana na maumbile ya wanaume. Pia tabia za wanawake kuhusiana na ngono ni tofauti sana na tabia za wanaume kuhusiana na ngono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaume wengi wana tabia ya kuchepuka sana na mara nyingi wanaweza wakavitoa virusi nje wakavileta kwenye ndoa zao kwa wanawake ambao wametulia; hilo halibishaniwi. Kwa hiyo, nitoe rai kwa wanaume wenzangu kujipanga sana kwenye eneo hili la kuchepuka, kuachana na michepuko, lakini pia kupima afya zetu, kupima hali zetu lakini pia kupima hali za wenza wetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale Waislamu wenzangu, tunapewa fursa ya kuoa wake hadi wanne; kuliko kuchepuka na watu usiowajua, unawakuta mtaani huko, ni bora ukapima na ukajiridhisha kwamba unayekwenda kumuoa yuko salama, ukatulia na wake zako wanne. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimewataja Mheshimiwa Mgeni, Mheshimiwa Khadija na Mheshimiwa Fredy.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Serikali ina mikakati gani ya kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI katika Jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Majibu kwa kifupi. Wako wengi na muda umekwenda.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali lake ni refu kidogo; tuna mikakati gani ya kupunguza maambukizi mapya? Mikakati tuliyonayo ni mingi sana. Mkakati mkubwa wa kwanza ni kinga, kuzuia watu wasipate maambukizi ya UKIMWI kwa kutoa Elimu ya Afya kwa Umma.

Mkakati wa pili, ni tiba ambapo tunatumia zaidi ya kliniki zaidi ya 2000 za *CTC (Care and Treatment Clinics)* ambazo zimetapakaa nchi nzima mpaka kwenye ngazi za Vituo vya Afya kwa ajili ya kutoa dawa za *ART (antiretroviral therapy)* dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI, tukiamini kwamba watu ambao wanatumia dawa, wanapungua *virulence,* wanapungua kiwango ambacho wanaweza wakaambukiza. Kwa hiyo, hata ikitokea bahati mbaya akafanya ngono ambayo siyo *protected* anaweza asimwambukize *partner* wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, tuna mkakati wa kuongeza sasa idadi ya watu ambao tunawatibu, kwamba kila atakayepimwa na kubainika na Virusi vya UKIMWI kuanzia Oktoba, 2016 atatibiwa hapo hapo, ataanza kupata dawa za kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mkakati mpya wa kisasa ambapo tumehama sana kwenye mikakati ambayo ipo *preventive based* tunahamia kwenye *treatment based,* kwamba badala ya kutoa tu kinga sasa tunatoa tiba zaidi. Kwa kufanya hivi, taratibu tutapunguza maambukizi mapya kwa kiasi kikubwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgeni. Waziri subiri kidogo, maana wako wengi utamalizia wewe nondo zako. *(Kicheko)*

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ilitoa elimu na tamko kuwa wanaume ambao hawajafanyiwa tohara wana maambukizo zaidi. Je, ni Mkoa upi ulioelimika na wanaume wengi kufanya tohara kwa hiari zao ili kuzuia kuambukiza maradhi ya UKIMWI?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli nakubaliana na yeye kwamba kumekuwa kuna makabila mengi nchini ambayo *traditionally* hawapendi kufanya tohara ya kukata, wana tohara nyingine ambazo wanafanya za elimu na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua hilo na ndiyo maana tumeweka msisitizo sana katika suala hili. Kwenye *Country Operational Plan* ya mwaka huu tumepewa takribani milioni 526 za Kimarekani na Mfuko wa UKIMWI wa Rais wa Marekani *(PEPFAR).* Hizo pesa ndani yake pamoja na kuongeza watu 360,000 kwa ajili ya kuwapa dawa za *ART*

lakini pia tutahamasisha na kuimarisha mkakati wetu wa kuwafanyia tohara wanaume katika mikoa ambayo *predominantly* hawapendi kufanya tohara ya kukata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fredy, jiandae Mheshimiwa Msabaha na Mheshimiwa Oliver.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa niulize swali moja la nyongeza. Ugonjwa wa UKIMWI siyo tishio kwa maana ya kuua, tishio kubwa ni magonjwa nyemelezi. Kwa bahati mbaya Serikali imekuwa ikinunua dawa hasa hasa kwa ajili ya kufumbaza Virusi vya UKIMWI aina ya *TLA (Tenofovir, Lamivudine* na *Efavirenz*). Je, ni lini Serikali itaanza kununua dawa kwa ajili ya magonjwa nyemelezi (*Opportunistic Infections -OI drugs)* hasa hasa *Azithromycin, Fluconazole* na *Co-trimoxazole?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, Mheshimiwa kwa kifupi sana, leo tumetoa *bonus* ya maswali. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inanunua dawa za *Opportunistic Infections* lakini siyo kwa kiwango ambacho tunanunua dawa hizi za UKIMWI za moja kwa moja kama hizo anazosema Mheshimiwa Mbunge za *Tenofovir, Lamivudine, Zidovudine, Efavirenz* na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upungufu tulionao sasa hivi tunaboresha kwa ujumla wake mfumo wa kutoa dawa nchini. Kwa hivyo, kadri mfumo wa dawa utakavyoboreka, dawa za kutibu magonjwa nyemelezi pia na zenyewe zitaongezeka kuwepo katika vituo vyetu. Kwa hivyo, ni lini, ni kadri tunavyoendelea kuboresha ndivyo ambavyo tutaendelea kuwa na dawa hizi kwenye vituo vyetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Msabaha, Mheshimiwa Oliver, Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Sugu wajiandae.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Mwenyezi Mungu akupe wepesi katika siku hii ya leo kwa sababu Wabunge umewafurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, kuna watu wanafanya makusudi kabisa kuambukiza wenzao ugonjwa huu. Mtu anajua kama ni muathirika wa UKIMWI lakini anambukiza watu kwa makusudi hata watoto wadogo ambao ni wanafunzi wa vyuo. Je, Serikali ina mikakati gani kwa hawa ambao wanafanya maambukizi ya makusudi kwa wanafunzi wa vyuo na hata kwa ambao hawajaambukizwa maradhi haya? Naomba tamko la Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Bunge lako Tukufu palitungwa sheria ambayo inatoa adhabu kwa watu ambao wataambukiza wengine Virusi vya UKIMWI kwa makusudi huku wakijua kwamba wana Virusi vya UKIMWI. Kwa hivyo, ili sheria hii iweze kufanya kazi ni watu kuripoti kwamba wameambukizwa Virusi vya UKIMWI kwa makusudi. Watakaporipoti, mkondo wa sheria utafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, kwanza watu wenyewe wapime, kwa mfano wewe unazungumzia mabinti, maana yake mabinti wapime wajue hali zao. Wakishajua hali zao hata ikitokea ameambukizwa na mtu ambaye hakupima naye anaweza akasema wewe ndiyo umeniambukiza kwa sababu mimi nilikuwa sina maambukizi. Kwa hivyo, wapime wajue hali zao na waweze kutumia kinga kama hawawezi

kuacha kufanya ngono, lakini kama wanaenda kuoana basi wapime kila mtu ajue hali wakate wanaoana ili wasiambukizane bila kujua.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Oliver, Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Sugu wajiandae.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Nina swali dogo la nyongeza. Kwa nini Serikali isiwezeshe lishe kwa kaya duni ambazo zinatumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali fupi, jibu fupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hatuna mpango wa kuwezesha chakula kwenye kaya duni au kaya yoyote ile. Tunaamini wagonjwa na watu wengine wanapaswa kuhudumiwa na familia zao. Hata hivyo, tunatoa dawa ama kemikali ambazo zina *nutritive effect*, zina *effect* ya kuongeza lishe kwenye miili ya wagonjwa wanaotumia dawa hizi. Kwa hiyo, tunawapo *multivitamins* na dawa nyingine inatosheleza kwa kweli kuhimili mikikimikiki ya *ART*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Sugu ajiandae.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa ugonjwa wa *TB* unaenea kwa hewa na sanasana naona Wizara inahamasisha sana watu kujikinga na UKIMWI lakini sijaona wanaweka nguvu sana kwenye ugonjwa wa *TB* na umeenea kwa kasi sana. Ni lini Serikali itatoa hamasa na kuwajulisha watu ugonjwa wa *TB* kuwa ni mbaya sana kwa vile huenea kwa hewa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa Kifua Kikuu ama *Tuberculosis* unaibuka tu kwenye mwili wa mwanadamu, pale ambapo kinga yake imeshuka. Ndiyo maana sasa unauona upacha wa maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, UKIMWI pamoja na Kifua Kikuu, sio kwamba ugonjwa haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hata sisi wazima na tuna afya tuna vimelea vya *Mycobacterium tuberculosis* kwenye miili yetu lakini havitajionyesha mpaka tutakufa navyo kama hatutoshusha kinga za mwili wetu. Kwa hiyo, kwanza tuepuke maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, lakini pili tuwe na tabia ya kupima afya zetu kwa kweli ili tuweze kudhibiti magonjwa kama haya kabla hayajatokea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sugu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri amesisitiza mara kadhaa kwamba tuwe na desturi ya kupima, ni kitu kizuri kwa sababu UKIMWI bado upo na *sometime* unaona kama umezoeleka hivi. Ni kwa nini sasa vile vipimo *(disposable)* haviko kwenye maduka ya dawa ya kawaida ili hayo maelekezo ya Waziri anayoyasema kwamba tuwe na desturi ya kupima iwe rahisi? Kwa sababu yale mambo ya kusema kwamba mtu atazimia ni ya kizamani. Ni vizuri vipimo vya UKIMWI viwe *available* madukani kama ilivyo kwa vipimo vya sukari, *pressure* na kadhalika ambavyo viko *available* madukani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni swali zuri na nieleze tu kwamba, katika hizi *USD* milioni 526 tulizopewa na Serikali ya Marekani kwenye mwaka huu wa fedha unaokuja, tumeweka mkakati wa kufanya majaribio ya *self-test* hiyo unayoisema. Kwa hivyo, tutaanza majaribio hayo, tunakwenda kisayansi, hii siyo blaa-blaa ya siasa mzee, tunakwenda kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunafanya majaribio tuone hasara na faida zake, tukijiridhisha kwamba ni kitu ambacho tunaweza tukakifanya ndiyo tuna *launch* sasa *scale up project* kwa nchi zima. Kwa hivyo, kwa mwaka huu tunafanya majaribio na ni hatua nzuri kwa sababu zamani tulikuwa hata tunaogopa kuruhusu watu kupimwa bila kuwa na ushauri nasaha kutoka kwa wataalam kwa kuepuka mambo mengine ambayo yangeweza kuibuka.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu, sasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nataka kutoa ufafanuzi kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Khadija Nassir kwamba tuna mikakati gani ya kuzuia maambukizi mapya. Kati ya mkakati mkubwa ambao tumeutekeleza na tunaendelea kutekeleza katika kupunguza maambukizi mapya ya VVU ni kupunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili tumefanikiwa sana, asilimia 92 ya vituo vyetu vya huduma takribani 5,200 vinatoa huduma ya kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Takribani wanawake zaidi ya asilimia 90 wote wanaohudhuria katika kliniki ambao ni wajawazito wameweza kupata huduma wale ambao wamekutwa na maambukizi. Tumefanikiwa sana Tanzania, kwa sababu ya mkakati huu, tumepunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kutoka watoto 14,000 hadi watoto 6,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo mkakati mkubwa na niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yetu, katika majimbo yetu, tuwahimize wanawake wajawazito mara tu wanapojigundua kwamba ni wajawazito waende kliniki lakini pia wapime UKIMWI kwa sababu

wataweza kuzaa watoto ambao hawatakuwa na maambukizi ya UKIMWI. Niliona nilisisitize hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri, Wizara hii ina bahati, Naibu na Waziri wake wote wazuri na wataalam na mnafanya kazi vizuri.

Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri liko suala la tohara, yako maeneo Tanzania jamii hutenga watu ambao wamefanya tohara. Sasa, kwa mkakati uleule wa kuzuia ukeketaji wa watoto wa kike na hii iwe na *affirmative action* ya kuelimisha jamii umuhimu wa tohara. Kuna maeneo mengine hata wanasiasa wanatengwa sasa sijui wanawajua vipi. *(Kicheko)*

Tunaendelea Mheshimiwa Ngonyani.

Na. 433

**Mgao wa Dawa – Kituo cha Afya cha Mji Mwema Songea**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Kituo cha Afya cha Mji Mwema katika Manispaa ya Songea kinahudumia watu zaidi ya laki mbili lakini kinapata mgao wa dawa sawa na vituo vingine vya afya:-

(a) Je, Serikali ina mpango wa kukiongezea dawa kituo hiki ili kipate mgao wa dawa na vifaa tiba kama Hospitali ya Wilaya?

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha vifaa vya upasuaji katika Kituo cha Afya cha Mji Mwema?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na

Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya mgawanyo wa fedha za dawa kulingana na idadi ya watu wanaopata huduma katika kituo husika. Takwimu za Wizara za mwaka 2015 zinaonesha kituo hicho kinahudumia wananchi 20,000. Kama kuna mabadiliko ya idadi ya wananchi wanaopata huduma katika kituo hiki ni vyema takwimu hizo ziletwe Wizarani na Mganga Mkuu wa Wilaya husika ili marekebisho yaweze kufanyika. Kwa kuwa hiki ni Kituo cha Afya, hakitapata mgao kama Hospitali ya Wilaya mpaka pale ambapo kitapandishwa hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kukamilisha upatikanaji wa vifaa vya upasuaji wa Vituo vya Afya nchini kikiwemo cha Mji Mwema chini ya mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN).* Mpango huu ni wa miaka mitatu na umelenga kupunguza vifo vya akinamama kwa asilimia 20. Katika kipindi hicho cha 2015 – 2018, Vituo vya Afya nchini vitaboreshwa ili kutoa huduma za upasuaji hasa kwa akina mama ambao wameshindwa kujifungua kwa njia ya kawaida. Serikali pia itaboresha idadi ya wataalam na upatikanaji wa dawa hasa za mpango wa mama na mtoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Manispaa ya Songea haina Hospitali ya Wilaya lakini pia katika Manispaa ya Songea, wakazi wengi wanategemea Kituo cha Afya cha Mji Mwema na kituo hicho hakina gari la wagonjwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta gari kwa ajili ya wagonjwa ili kurahisisha kutoa huduma pamoja na kurekebisha jengo la upasuaji ili kuweza kwenda sawasawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ina mkakati gani wa kuweka Kituo cha Damu Salama katika Kituo cha Afya cha Mji Mwema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la kwanza kuhusu *ambulance*, kama ambavyo tumekuwa tukisema hapa Bungeni kila siku siyo jukumu la Wizara ya Afya. Kimsingi ni jukumu la Halmashauri husika kwamba katika vituo wanavyovimiliki na wanavyoviendesha, kama kuna mahitaji ya *ambulance* basi Halmashauri husika iweke katika vipaumbele vyake iweze kununua *ambulance* hizo na kuzipeleka kwenye vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya sisi Wizara ya Afya na naona sasa kinatuletea shida, tunaomba kwa wahisani watupe *ambulance* katika maeneo ya kipaumbele kama eneo la kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto, tukipata ndiyo tunatawanya kwenye Majimbo na kwenye Halmashauri kadri ambavyo tutaweza kufanya hivyo, lakini sio jukumu letu. Kwa hiyo, natoa rai kwake na kwa Halmashauri zote nchini kuweka kipaumbele cha kununua *ambulace* katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili linahusu damu salama. Mpaka sasa tuna upungufu wa kuwa na vituo vikubwa vya kanda vya damu salama katika mikoa saba nchini, Mikoa ya Geita pamoja na Arusha wameonesha uwezekano wa kujenga vituo vyao wenyewe. Mikoa ambayo imebaki tumeweka kwenye bajeti, mwaka jana tuliweka shilingi bilioni mbili bahati mbaya hatukufanikiwa kukamilisha, mwaka huu pia kwenye bajeti hii tumeweka tena shilingi bilioni mbili. Malengo yetu kwa kweli ni kuhakikisha mikoa hii ukiwemo Mkoa wa Ruvuma pale Songea tunajenga kituo kikubwa cha Damu Salama ili kuokoa Maisha ya Watanzania wenzetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Raisa ajiandae.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hospitali ya Rangi Tatu, Mbagala ina upungufu mkubwa wa dawa na huwa zinachelewa kuletwa katika hospitali ile. Vilevile tunawadai *MSD* dawa zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 300. Je, Wizara itatusimamia dawa zile zipatikane ili tuweze kutoa huduma hasa ikizingatiwa tunatoa huduma mpaka maeneo ya Mkoa wa Pwani maeneo ya Mkuranga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kituo hiki cha Rangi Tatu nakifahamu vizuri kwa sababu mdogo wangu pale ndiyo *in charge* wa kituo kile, sidhani kama Mheshimiwa Issa anajua, kwa hiyo nafahamu changamoto hiyo na kwamba kina wateja wengi sana, maana yake analalamika halali kwa kufanya kazi kwa bidii kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakachokifanya, nitafanya kazi kwa ukaribu na Mheshimiwa Mangungu kufuatilia tuone kama kweli wanadai shilingi milioni 300 na kama wanadai basi waweze kupata huduma hiyo ya dawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Raisa, wajiandae Mheshimiwa Hussein Nassoro na Mheshimiwa Devota.

**MHE. RAISA ABDALLA MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri wanayotoa Wizara ya Afya mara nyingi wanapoulizwa maswali hapa Bungeni nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la msingi ni kwamba kunahitajika vifaa tiba katika hospitali za Serikali. Sasa pamoja na vifaa tiba, kuna kitu muhimu ambacho

kinatakiwa na Watanzania katika Hospitali hasa za Serikali nacho ni kauli nzuri ya wahudumu na wafanyakazi katika hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Waziri na Naibu Waziri kwamba suala hili halipatikani katika katika Hospitali zetu za Serikali. Ama ukienda hospitali za binafsi jinsi wanavyofanya biashara zao wanawanyenyekea watu, lakini hospitali hizi za wanyonge hilo halipatikani. Je, Mheshimiwa Waziri anatuambia vipi kuhusu wafanyakazi ambao wanatoa kauli ambazo haziridhishi kwa Watanzania? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza natambua kazi nzuri na kubwa inayofanywa na wataalam wanaotoa huduma kwa watu wetu hapa nchini. Napenda sisi kama viongozi tutambue kazi kubwa wanayoifanya kwa kujitoa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natambua kuwa kuna baadhi ya wafanyakazi ambao wana changamoto hizo anazozisema Mheshimiwa Raisa kwamba wana lugha mbaya, wanashindwa kuhudumia watu vizuri na *customer care* ni mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwamba wataalam wote kwenye sekta ya afya wale wachache ambao bado hawajabadilika, huu ni wakati wa kubadilika. Kwa sababu kwa kweli tukipata taarifa za mtaalam ambaye amem-*treat* vibaya mteja wetu huwa tunachukua hatua bila kulaza damu. Kwa hiyo, nitoe rai wasiombe nikawakuta na tuhuma hizi kwa sababu nitawapeleka kwenye Baraza lao la Kitaalam waweze kuchukuliwa hatua za kitaaluma. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hussein Nassor jiandae Mheshimiwa Devota.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mimi Mbunge wa Jimbo la Nyang'wale niliweza kujitolea na kujenga zahanati na kuikamilisha katika Kijiji cha Mwamakiliga na kwa kuwa niliweza kujitolea na kujenga wodi mbili na chumba cha kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya ambayo ni Hospitali ya Wilaya ya Nyang'wale, nimeweza kuyafikisha majengo hayo kiwango cha asilimia 75 na nimekwama. Je, Serikali inasaidia vipi sasa kuweza kuifungua ile zahanati ya Mwamakiliga ili iweze kufanya kazi na kukamilisha majengo hayo yaliyo katika Kituo cha Afya Kalumwa ili yaweze kufanya kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Hussein Nassoro Amar kwa kujitoa kiasi hicho kwa ajili ya wananchi wa Nyangh'wale. Nimwombee dua Mungu apokee swaumu yake katika Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa sadaka hiyo kubwa aliyoitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimhakikishie kwamba sisi tutakuwa pamoja naye, bahati mbaya sikufika pale Kalumwa wala Mwamakiliga nilipokuja kwenye ziara ya Mkoa wa Geita, lakini baada ya Bunge hili nina ziara tena ya kuzunguka mikoani na nitapita Mkoa wa Geita na mahsusi nitafika kwako na kwa Mheshimiwa Musukuma nina ahadi yangu naikumbuka. Nitakapofika pale, nitaongea na wataalam wale tujue ni nini cha kufanya kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ili kuweza kuunga mkono jitihada nzuri alizozionyesha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Devota.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Matatizo ya afya katika Mkoa wa Songea yanafanana kabisa na matatizo ya afya katika

Hospitali ya Mkoa Morogoro ambapo licha ya kazi nzuri inayofanywa na Madaktari katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro lakini hospitali ile inaelemewa na wagonjwa wengi. Kwa mwezi mmoja Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro inatibu zaidi ya wagonjwa 15,000. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kupeleka vifaa muhimu kama *MRI, CT-Scan* na *X-ray machines* za kisasa ili kuwapunguzia mzigo wagonjwa ambao wanalazimika hivi sasa kwenda Muhimbili kwa matibabu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini Mheshimiwa Mohamed Abood kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye hospitali ile lakini pia kwa kutumia pesa zake za mfukoni kuweza kununua baadhi ya vifaa tiba ambavyo vinatumika katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumwaga sifa hizo kwa Mheshimiwa Abood, naomba nijibu sasa swali la Mheshimiwa Devota Minja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango mkubwa kupitia mradi wake wa *ORIO* wa kupeleka vifaa tiba kwenye Hospitali za Mikoa nchini, Hospitali za Wilaya na baadhi ya vituo vingine maalum vya kutolea huduma za afya nchini. Mradi huo ulisuasua mwaka jana kwa sababu tulikuwa hatujalipa *counterpart funds* kwa Serikali ya *Netherlands* ambao ndiyo wafadhili wa mradi ule. Sasa tumeshaanza kukamilisha sehemu yetu ya fedha ambazo tunapaswa kulipa ili mradi uanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika baada ya miezi mitatu mradi huu utaanza kutekelezwa. Mradi huu ukitekelezwa, tutaweza kupata *CT-Scan*, MRI, *Ultra-sound*, *digital X-rays* na vifaa vingine vingi vya kufanyia uchunguzi

wa magonjwa kwa ajili ya hospitali zetu hapa nchini. Sina hakika mgao umekaaje mahsusi na Hospitali ya Rufaa ya Morogoro, lakini naamini kwa vile ni kati ya hospitali kubwa hapa nchini inawezekana ikapata badhi ya vifaa hivi vikubwa ambavyo vinatarajiwa kuja lakini nitaangalia na akipenda nimpe taarifa nitampa baadaye.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hamad Omar, Wizara ya Fedha.

Na. 434

**Ukwepaji wa Ulipaji wa Kodi**

**MHE. JUMA HAMAD OMAR** aliuliza:-

Kuna wakati mwananchi anapaswa kulipa kodi zaidi ya thamani ya bidhaa au kifaa alichonacho:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba yanapotokea hayo yanashawishi mlipa kodi husika kulipa kwa njia ya panya au kukwepa kodi?

(b) Je, ni kiasi gani cha misamaha ya kodi kimekuwa kikitolewa na Serikali kwa kipindi cha miaka kumi nyuma na ni nini athari zake katika uchumi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi kuu zinazotozwa kwenye bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi ni Kodi ya Ongezeko la Thamani yaani *VAT,* Ushuru wa Bidhaa na Ushuru wa Forodha. Kiwango cha Kodi ya *VAT* kwa bidhaa

zote zinazostahili kulipiwa *VAT* ni asilimia 18 bila kujali kuwa bidhaa imeagizwa kutoka nje ya nchi au imezalishwa hapa nchini. Aidha, viwango vya ushuru wa bidhaa kwa bidhaa nyingi, isipokuwa magari, hutumia viwango maalum (*specific rate)* kulingana na aina ya bidhaa. Kwa mfano, bia hutozwa Sh.729 kwa lita, mafuta ya petroli Sh.339 kwa kila lita na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya Ushuru wa Forodha vinavyotumika hapa nchini ni vile vya ushuru wa pamoja wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushuru huu unatumia viwango vinavyozingatia kiwango cha uchakatwaji wa bidhaa husika. Bidhaa za mtaji na baadhi ya malighafi hutozwa ushuru wa asilimia sifuri, bidhaa zilizochakatwa kwa kiwango cha kati na vipuri hutozwa asilimia 10 na bidhaa za mlaji hutozwa asilimia 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, mfumo wa kodi kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchini unazingatia Sheria ya *VAT* na Sheria ya Ushuru wa Pamoja wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa minajili ya kulinda mazingira pamoja na viwanda vya ndani, kuna baadhi ya bidhaa ambazo zinatozwa Ushuru wa Bidhaa kwa zaidi ya asilimia 25. Mfano, sukari asilimia 100 au Dola za Marekani 460 kwa tani moja kwa kutumia kiwango chochote kilicho kikubwa zaidi na magari yaliyotumika kwa zaidi ya miaka kumi tangu tarehe ya kutengenezwa hutozwa ushuru wa ziada wa uchakavu wa asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ni kweli kuwa kuna baadhi ya bidhaa ambazo zinaweza kutozwa kodi zaidi ya bei ya kununulia ikiwa zitaangukia katika kundi hili la kulinda mazingira pamoja na viwanda vya ndani. Aidha, ukwepaji kodi unaofanywa na baadhi ya waagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi unatokana na tabia ya waagizaji wenyewe kukosa uzalendo na si vinginevyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha msamaha wa kodi uliotolewa na Serikali katika kipindi cha miaka kumi iliyopita ni shilingi trilioni 11.8 ikiwa ni wastani wa shilingi trilioni 1.18 kwa mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi wa swali langu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Serikali inapoteza kiasi cha shilingi za Kitanzania trilioni 1.18 kila mwaka. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Idara ya Afrika ya *IMF* kuhusu *effect* ya hizi *exemptions* kwa uchumi wa nchi ambazo ziko Kusini mwa Jangwa la Sahara, imebainika katika ripoti hii kwamba Tanzania ikiwa ni moja ya nchi hizo inapoteza kiasi cha Dola bilioni 1.2 hadi Dola bilioni 2.2 kwa wastani kwa mwaka ambapo hiyo ni sawasawa na kiasi cha shilingi za Tanzania trilioni 2.2 mpaka kwenda kwenye shilingi trilioni 4.6. Nataka kujua ni takwimu zipi sahihi za Waziri au za utafiti huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ripoti hii ya uchunguzi imebainisha kwamba kivutio cha misamaha ya kodi sio tena kivutio kikubwa kwa maana ya kuwa-*attract* wawekezaji kuingia katika nchi. Yako mambo matatu ambayo sasa hivi wawekezaji wanaangalia sana yakiwa ni kipaumbele. Kwanza, ubora wa miundombinu. Pili, sera sahihi za fedha zinazotabirika (*predictable financial and monetary policies).* Tatu, utawala bora na utulivu wa kisiasa (*good governance and political stability). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, kwa sababu *tax incentive* siyo tena kipaumbele au vigezo wanavyoviangalia wawekezaji, haoni kwamba *time* imefika sasa ya kubadilisha ile Sheria ya Uwekezaji hasa Kifungu cha 38 na kubadilisha sheria

zinazoanzisha Maeneo Tengefu (*Economic Processing Zone, Sspecial Economic Zone and Export Processing Zones)* ili misamaha hiyo itolewe kidogo sana kuliko ilivyo sasa ambapo inachukua karibu asilimia 8.3 ya bajeti yote ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, naomba nisema takwimu nilizozisema mimi ni halali kabisa kwa sababu zimetoka katika takwimu za Serikali na naomba aziamini. Hatuna sababu ya kudanganya takwimu hizo kwa sababu tunajua madhara ya mishamaha hii ya kodi kwa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, nakiri kwamba ni sahihi kivutio cha kodi sio kivutio tena lakini nimwambie tu Tanzania yetu ni nchi ya mfano katika Bara letu la Afrika na dunia kwa ujumla kwa sera zake za *monitory* pamoja na *fiscal policies* ndiyo maana wawekezaji wanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilikumbushe Bunge lako, ni juzi tu wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Viwanda pamoja na bajeti ya Wizara ya Fedha, Waheshimiwa Wabunge hawa hawa walikuwa wakilalamika kwamba zipo *tax incentive* ambazo tunashindwa kuzitoa na wawekezaji wanashindwa kuja nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii napata shaka kidogo na swali hili la Mheshimiwa Omar, lakini kama Serikali tunajua na tunafahamu misamaha hii ya kodi tunaitoa kisheria na tunaangalia mazingira ya kiuchumi ya Taifa letu, nani anakuja na kufanya nini katika uchumi wetu, lakini pia kijamii ana *impact* gani mtu huyu tunayempa msamaha huu na sheria zetu pia tunaziangalia kwa uhakika kabisa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko halafu tunaendelea.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Nina swali dogo tu la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri. Ulipaji wa kodi unategemea uwepo wa ofisi za *TRA* katika maeneo mbalimbali. Nimekuwa nikiuliza zaidi ya mara mbili, sisi Halmashauri ya Mji wa Kasulu tumeshatoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za *TRA* na tumewapa bure. Swali langu, kwa sababu bajeti imepita kwa kishindo, ni lini ofisi ya *TRA* itajengwa katika Mji wa Kasulu ili kuhudumia Wilaya nne zilizopo katika Mkoa wa Kigoma za Kakonko, Kibondo, Buhigwe na Uvinza? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza yeye pamoja na Halmashauri yake kwa kutoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za *TRA* katika Wilaya ya Kasulu, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niseme Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitoa *commitment* kwamba ofisi hizi zitajengwa na nirudie kusema na niagize ofisi yetu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania wahakikishe ndani ya mwaka huu wa fedha 2017/2018, ofisi hizi zinajengwa katika Wilaya ya Kasulu ili kusogeza karibu huduma hizi kwa wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Naona *pressure* kubwa na leo nimesema ni *bonus* ya maswali, Mheshimiwa Kabati na Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo tu la nyongeza japokuwa kidogo linafanana na muuliza swali aliyepita. Ili kurahisisha ukusanyaji na ulipaji kodi ni kwa nini *TRA* isiweke vituo katika kila Halmashauri ya Wilaya ili kupunguza usumbufu mkubwa wanaopata walipa kodi? Kwa mfano, ukichukulia Mkoa wetu wa Iringa, jiografia

yake ni mbaya sana inawasabisha hata watu wengine kukwepa kodi kwa sababu tu vituo vya *TRA* viko mbali sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi na hakuna Taifa lolote linaweza kuendelea bila kukusanya mapato, tunafahamu kabisa hilo kama Wizara yenye mamlaka ya ukusanyaji wa mapato Tanzania. Hili la kuanzisha ofisi kila Halmashauri, nilishawahi kujibu ndani ya Bunge lako Tukufu kwamba kuanzishwa kwa ofisi huwa kuna tathmini ambayo huwa inafanyika kuangalia *cost and benefit analysis* ya kuanzisha ofisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Mbunge, tutafanya uhakiki na tathmini hiyo kujua kama kuna uhitaji mkubwa wa kuweka ofisi hizi katika kila Halmashauri ndani ya Mkoa wa Iringa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Tanzania ndiyo nchi ambayo inaongoza kwa viwango vya juu vya kodi ukilinganisha na nchi ya Kenya, Rwanda na Uganda. Serikali ina mkakati gani wa kupunguza viwango hivi kwa sababu vinaathiri sana wafanyabiashara hasa wadogo wadogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kodi za forodha ambazo zinatozwa huwa tunafuata mfumo wa kodi wa Afrika Mashariki. Kwa hiyo, si sahihi kusema Tanzania tunaongoza kwa viwango vikubwa vya kodi. Jana tu tumepitisha bajeti kuu ya Serikali, tumeona ni kwa kiwango

gani tumeweza kupunguza na kuondoa kodi ambazo zimekuwa ni kero kwa wafanyabiashara wetu hasa wafanyabiashara ndogondogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *TRA* ni chombo cha Muungano na katika suala linalowakera Wazanzibari kwa ujumla wake ni pale wanapotozwa kodi Zanzibar na wakiingia na mizigo yao Tanzania Bara wakatozwa tena kodi mara ya pili. Suala hili limekuwa ni kero moja kubwa sana na Serikali imekuwa ikilipiga danadana kwa kuliingiza kwenye misamiati kero za Muungano, mchakato lakini halifikii mwisho. Naomba Waziri anijibu suala hili la Wazanzibari kutozwa kodi Zanzibar na wanapoingia Bara na mizigo yao wakatozwa tena kodi ni lini litamalizika na kupatiwa ufumbuzi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimwambie Serikali haina dhamira ya kuwapiga danadana wafanyabishara wa Zanzibar. Nimekuwa nikisema hapa Serikali yetu iko *committed* katika kuwalea wafanyabiashara wetu hasa sekta binafsi kwa sababu tunajua sekta binafsi ni injini ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utozaji wa kodi mara mbili na naomba niliweke vizuri sio kodi mara mbili ni kutozwa kodi ambayo iko tofauti kati ya mifumo miwili ambayo inatumika Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara. Katika hili, Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na *ZRB* wanashughulikia tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisimwambie ni lini kwa sababu ni suala la kimfumo, kipindi watakapokubaliana kutumia mfumo mmoja, tatizo hili litaondoka. Hili linafanyika

ili kulinda tu ile *fair competition* katika soko letu na hili linafanyika kwa nia njema kabisa.

**MWENYEKITI:** Washeshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano, Mheshimiwa Deo Ngalawa.

Na. 435

**Mawasiliano ya simu**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Tarafa ya Mwambao katika Wilaya ya Ludewa yenye Kata za Lupingu, Lifuma, Makonde, Kilindo na Lumbila hazina mtandao wa mawasiliano ya simu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea wananchi wa maeneo hayo mtandao wa mawasiliano ya simu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote inatambua tatizo la huduma ya mawasiliano katika maeneo ya Tarafa ya Mwambao. Kwa kulitambua hilo, Serikali kupitia Mfuko huo wa Mawasiliano kwa Wote imeainisha maeneo ya Vijiji vya Kata za Lumbila, Kilindo, Makonde na Lupingu na kuyaingiza katika zabuni iliyotangazwa tarehe 20 Februari, 2017. Zabuni hiyo ilifunguliwa tarehe 27 Aprili, 2017. Aidha, baada ya tathmini ya zabuni kukamilika Kata za Lumbila, Kilindo, Makonde na Lupingu zimepata mtoa huduma wa kufikisha huduma ya mawasiliano.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini hasa Mkandarasi ataanza kujenga minara hiyo ya mawasiliano ya simu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, baada ya majibu hayo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, je, wananchi waishio Tarafa ya Mwambao mpakani mwa nchi ya Malawi, ni lini wataanza kupata mawasiliano hayo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumeongea naye siku za nyuma, taratibu za manunuzi siyo rahisi sana mimi kama Waziri kuja hapa kutamka, kwa sababu siwezi kuziingilia taratibu za manunuzi. Taarifa niliyopewa kutoka kwenye Bodi imeniambia kwamba Mkandarasi amepatikana kwa ajili ya hayo maeneo manne lakini hawawezi kunitajia mpaka taratibu zile zingine zikamilike za kum-*engage* huyo Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge, asubiri taratibu hizo za manunuzi zitakapokamilika ambazo nina uhakika hazitachukua muda mrefu kabla ya mwezi huu kuisha tutamjulisha lini kwa sababu inakuwa ndani ya mkataba wa yule Mkandarasi, anatakiwa aanze lini na akamilishe lini, tutakapokamilisha hilo tutamjulisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la lini mawasiliano yataanza kupatikana nalo litajibiwa vizuri zaidi baada ya ule mkataba kati ya *UCSAF* na Mkandarasi kukamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Genzabuke, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Chikota, Mheshimiwa Profesa Jay.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Katika Jimbo la Babati Mjini, vijiji vya Himiti, Chemchem na Imbilili havina mawasiliano na hili nililiandikia kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii akanijibu kwamba, anafanya maongezi na watu wa *Halotel* mwezi wa Tatu mwaka huu minara ya *Halotel* ingeweza kusimikwa katika vijiji hivyo, lakini hadi sasa hakuna kazi yoyote inayoendelea. Naomba nipate kauli ya Serikali, ni lini mazungumzo yao na watu wa *Halotel* yatakamilika ili wananchi wa Jimbo la Babati Mjini katika vijiji nilivyovitaja vipate mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo yanaendelea na eneo ambalo tuna tatizo nalo ni eneo la kodi ya vifaa ambavyo vinatakiwa vitumike katika kukamilisha haya mawasiliano. Namwomba tu maadam bajeti wameipitisha jana na kuna baadhi ya kodi tumeziondoa, nina uhakika mazungumzo haya yatakamilika karibuni na yakishakamilika tutakuja kumwambia watu wa *Halotel* watakamilisha lini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali moja, Mkoa wa Kigoma Wilaya Tano zinapakana na nchi jirani ya Burundi na kati ya Wilaya hizo zina vijiji ambavyo vimepakana kabisa na nchi ya Burundi na wakati mwingine zinapata mawasiliano kutoka Burundi. Je, ni lini Serikali itakaa na makampuni ili kuweza kupeleka minara katika vijiji vya Kalalangabo, Mtanga na Kiziga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Wajiandae Mheshimiwa Msukuma, Mheshimiwa Chikota na Mheshimiwa Profesa Jay.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji hivyo vya

Kalalangabo namshukuru amenitajia hapa nimhakikishie tu kwamba katika zabuni itakayofuata ambayo mkazo mkubwa ni katika maeneo ya mpakani na zabuni inayofuata ni ya mwezi wa 10, vijiji hivyo tutavifikiria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mawasiliano mbali na simu, mawasiliano ni pamoja na barabara, wananchi wa Jimbo la Geita Vijijini Sengerema na Buchosa kumekuwa na kero kubwa sana ya *TANROAD* Mkoa wa Mwanza kuweka mzani kwenye barabara ya vumbi, kitendo ambacho hatukioni kwenye mikoa mingine yoyote Tanzania. Je, Waziri yuko tayari kutoa kauli ili mizani inayowekwa kwenye barabara ya vumbi ambayo ni mbaya iondolewe mara moja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Mbunge na ninachoweza kumwahidi ni kwamba nitalifanyia kazi suala hilo, nikalione hilo eneo, nijue kwa nini wameweka mizani katika barabara ya aina hiyo, baada ya hapo tutachukua hatua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota, ajiandae Mheshimiwa Profesa Jay.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika Jimbo la Nanyamba kuna kata saba ambazo hakuna mawasiliano ya uhakika ya simu, Kata ya Hinju, Nitekela, Nyundo, Mnima, Kitaya, Kilomba na Kianga. Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea mawasiliano ya simu wananchi wa maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naib Waziri, mikakati ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na Kijiji cha mwisho hicho cha Kianga, Kitaya, Nitekela na kadhalika nimhakikishie kwamba majina haya tumeyapata na bahati nzuri hayo maeneo anayoyaongelea nayo yapo katika maeneo ya mpakani ni maeneo ambayo yanatakiwa yapewe kipaumbele. Kwa hiyo, nimwahidi katika kwamba katika Zabuni inayofuata ya kuhakikisha vijiji vyote Tanzania tunapeleka mawasiliano, zabuni ya mwezi wa Kumi vijiji hivyo navyo tutavifikiria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Jaya, ajiandae Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Matatizo yaliyopo katika Jimbo la Ludewa yanafanana sana na matatizo ambayo yapo katika Jimbo la Mikumi. Matatizo ya mtandao wa mawasiliano ya simu, hasa kwenye Kata za Vidunda, Muhenda, Uleling'ombe pamoja na Tindiga lakini pia Kata ya Masanze hasa kwenye vijiji vya Munisagala na Chabima. Je, ni lini Serikali italeta mawasiliano haya ya simu katika kata hizi za Jimbo la Mikumi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani jibu alilolitoa jana la kuikataa bajeti ni kwamba labda mwaka huu wote tusiangalie katika eneo la Mikumi. Nitaomba tukutane, pengine ile aliikataa siyo kutoka rohoni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Nipende tu kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri katika Wilaya ya Igunga Kata ya Mwashiku, Vijiji vya Matinje, Buchenjegele, Ngulu na maeneo ya karibu pale, ni maeneo ambayo wanachimba dhahabu na wafanyabiashara wadogo wadogo wanapata

tabu sana katika kufanya *transactions* za fedha kupitia hii mitandao ya simu, biashara hii za dhahabu wanaifanya kwa muda mrefu sasa. Je, ni lini sasa Serikali itawapelekea mawasiliano ya simu kama mitandao ya *Vodacom, Airtel,* na mitandao mingineyo ili kuwarahisishia wananchi kutokutoka maeneo yale ya Vijiji vile vya Matinje kwenda mpaka Nzega au Igunga? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo aliyoyataja kwa uelewa wangu ni kwamba yana mawasiliano. Sasa nitapenda tukutane tujadiliane kwa kirefu, labda anaongelea mitandao ya ziada. Kama kuna eneo ambalo halina mtandao tuwasiliane, tukubaliane cha kufanya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Tabora Mjini, Kata ya Ikomwa maeneo ya Kapunze; Kata ya Kabila, maeneo ya Igosha; Kata ya Ndevelwa, maeneo ya Ibasa; na mengine ambayo kwa muda mrefu hayana mawasilino, *Halotel* inaonekana inasuasua hata kwenda kufanya *survey* tu maeneo yale. Sijui Serikali ina mkakati gani kuhakikisha hawa Mameneja wa Mikoa wa *Halotel* wanafanya kazi ipasavyo ili maeneo hayo yapatiwe huduma ya mawasiliano? Serikali ina mkakati gani kwa kuwa hiyo pesa inalipwa na Serikali kuhakikisha hawa Mameneja wa Mikoa wa *Halotel* wanafanya kazi yao kwa ufanisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa taarifa hiyo, lakin nataka tu niweke *record* sawa, Kampuni ya *Halotel* haijengi kwenye vijiji kwa

kutumia fedha za Serikali ni fedha zao ila tumekubaliana na Serikali kwamba tuwape unafuu fulani wa kupata *wayleave* bila kulipa fidia ili waweze kufikisha mawasiliano katika vijiji vingi zaidi Tanzania, tuliwapa vijiji 4,000. Kwa hiyo ni fedha zao siyo hela za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nimhakikishie kwamba tutaliangalia na hilo eneo, tuone kama *Halotel* wataweza kufikisha mawasiliano mapema au tuviingize hivi vijiji katika mpango wa Mawasiliano kwa Wote, ambapo hapo ndiyo tunatoa fedha za Serikali kwa makampuni ambayo yanashinda tenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana kwa juhudi zake za kufuatilia masuala ya wananchi wake na mkutano wetu uliotukutanisha mimi na Waziri wangu kuyaongelea haya masuala, nimhakikishie kwamba tutatekeleza yale ambayo tulikubaliana kwenye kikao pamoja na kwamba leo amerudia kuliuliza hilo, labda kwa sababu ni muda mzuri wananchi wasikie. Hata hivyo, tunatambua juhudi zake na kwa namna ambavyo amelifuatilia sana suala hilo ofisini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana swali letu la mwisho Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Mgumba.

Na. 436

**Kuongeza Ardhi ya Akiba kwa Wakulima Wadogo Wadogo**

**MHE. OMAR T. MGUMBA** aliuliza:-

Shamba Na. 217 lenye ukubwa wa hekta 63,000 lililopo katika Kata ya Mkulazi, Morogoro Vijijini limepata Mwekezaji Kampuni ya Mkulazi *Holding Company Limited* kwa ajili ya kuliendeleza kwa Kilimo cha Mazao mbalimbali na uwekezaji wa kiwanda cha sukari . Aidha, wakulima wadogo *(out*

*growers)* wametengewa eneo la hekta 3,000 tu na Wawekezaji hekta 60,000 kwa ajili ya shughuli zao:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ardhi ya akiba kwa wakulima wadogo kutoka hekta 3,000 kwenda hekta 23,000;

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kutenga hekta 3,000 tu itazalisha vibarua wengi wazawa badala ya kuwashirikisha katika uzalishaji ili kuinua hali zao za maisha pamoja na kuongeza Pato la Taifa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi anazofanya katika kuhakikisha wakulima wanapata maeneo ya kilimo, napenda kutoa taarifa kuwa, hekta 3,000 za wakulima wadogo wadogo zilizoainishwa na Mheshimiwa Mbunge ziko kwenye eneo la Matokeo Makubwa Sasa. Katika mpango huu inakadiriwa kuwa hekta 250,000 kwa ajili ya wakulima wadogo wa kibiashara na hekta 350,000 kwa ajili ya wakulima wakubwa wa kibiashara zitapatikana na zitalimwa zao la miwa na mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la Mkulazi ambalo liko kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge jumla ya hekta 63,000 zimepimwa na kutolewa Hati Miliki ambayo inamilikiwa na Serikali Kituo cha Uwekezaji (*TIC),* ambapo hekta 60,000 ni kwa ajili ya wakulima wa mashamba makubwa ya kibiashara ya uwekezaji na hekta 3,000 ni kwa ajili ya wakulima wa mashamba madogomadogo ya kibiashara. Wakulima wadogo watatoka kwenye vijiji vinavyozunguka eneo hilo la uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa uwekezaji mkubwa utatumia teknolojia ya kisasa na Kanuni bora za kilimo, kwa kufanya hivyo, maeneo ya wakulima wadogo yatachangia kwa kiasi kikubwa ukubwa wa eneo linalozalisha zao hilo, pia wingi wa ubora wa zao ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje na hivyo kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji huu hautazalisha vibarua bali utazalisha wakulima na wajasiliamali wengi, ambao watashiriki kikamilifu katika mnyororo wa thamani *(value chain)* wa zao husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgumba.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; swali langu kipengele cha (a) lilikuwa liko *straight forward* niliomba kwamba Serikali iongeze ardhi ya wakulima wadogo toka hekta 3,000 mpaka hekta 23,000, lakini kwenye majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri bado hakutoa jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa swali langu ilikuwa ni ardhi iliyotengwa kwa ajili ya wakulima wadogo ni ndogo, naiomba Serikali iongeze. Je, ni nini kauli ya Serikali katika suala hili kuongeza ardhi hiyo kutoka hekta 3,000 kwenda 23,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sSwali la pili; kwa kuwa, katika jibu la Serikali limesema imetenga ardhi ya ukubwa wa hekta 3,000 kwa ajili ya wakulima wadogo wa vijiji vinavyozunguka shamba hili la Mkulazi kwa maana ya Vijiji vya Kidunda, Chanyumbu, Usungura, Mkulazi katika Kata ya Mkulazi na Kijiji cha Kwaba katika Kata ya Matuli; na kwa kuwa, mradi huu ni miongoni mwa miradi mitano ya kielelezo ya Kitaifa, manufaa yake inawanufaisha Watanzania wengi. Je, Serikali itatenga ardhi kiasi gani kwa ajili ya wananchi

wengine nje ya vijiji hivi vitano wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki ili washiriki katika mradi huu wa wakulima wadogo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ombi lake la kwamba ardhi ile iongezwe mpaka hekta 23,000 kwa ajili ya wakulima wadogo, naomba nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli katika majadiliano ambayo yanaendelea kati ya *NSSF* na *PPF* ambao hasa ndio wanaomiliki Mkulazi *Holdings* tayari kuna mwelekeo kwamba ardhi ile itaongezeka ili wakulima wadogo waweze kuongezeka kwa wingi zaidi. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tayari hilo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusiana na swali lake la pili ni kwamba huu ni mradi wa Kitaifa na hivyo ingekuwa vema kama vijana na wananchi wengine Watanzania wakaweza kunufaika. Nimhakikishie kwamba tayari Ofisi ya Waziri Mkuu ya Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu wameweka mkakati wa kuhakikisha kwamba vijana wengi zaidi watanufaika katika mradi huo na watatengewa *blocks* pamoja na kupatiwa mafunzo ili waweze kushiriki vizuri katika kilimo cha miwa, vijana wale watatoka nchi nzima siyo Morogoro peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari kuna huo mpango wa kuhakikisha vijana wengi wanashiriki zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vijana wanapata elimu nzuri ya namna ya kuotesha miwa na kushiriki katika *value chain* nzima ya zao la miwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *bonus* imekwisha, sasa ni muda wa wageni. Wageni waliopo

jukwaa la Spika ni wageni watatu wa Naibu Spika wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kutoka Jiji la Dar es Salaam ambao ni Dkt. Sebastian Ndege, Ndugu Jijo Joseph na Ndugu Fatma Mahsen. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni Watatu kutoka Bunge la Uganda waliokuja kwa ajili ya mafunzo katika Bunge letu, *Guests from the Parliament of* Uganda *welcome to the Parliament of Tanzania.* *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni watatu wa Mheshimiwa Anastazia Wambura Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wasanii kutoka Jiji la Dar es Salaam Ndugu Lidya Mgaya, Ndugu Nice Mtunis na Ndugu Amin Mwinyimkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 56 wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi Mbunge, ambao ni wananchi wa Jimboni kwake kutoka Mlalo, Mkoa wa Tanga, karibuni Bungeni na jioni msiondoke kuna futari leo. *(Makofi)*

Vile vile wapo wageni 13 wa Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea ambao ni Mashekhe kutoka *The Islamic Foundation* kutoka Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na Sheikh Aref M. Nahdi - Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo ni Wanafunzi 70 na Mwalimu mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Jumuiya ya Wabunge Waislam ikishirikiana na *The Islamic Foundation,* Redio Iman na *TV* Iman, leo Jumatano wameandaa *Iftal* kwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Watumishi wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wageni wote watakaokuwepo Bungeni leo katika viwanja vya Bunge, wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti

**MWENYEKITI:** Jamani baada ya *bonus* kuna miongozo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Musukuma.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana, naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) kwa sababu ya muda tuko wengi nisiisome. Naomba mwongozo wako kuhusiana na suala linaloendelea kwenye Majimbo yetu, na suala hili tumekuwa tukililalamikia humu mara nyingi na Mawaziri kutoa kauli ambazo hazitekelezeki kule Majimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Majimbo yetu kunaendelea kupigwa minada ya ng'ombe, kitu ambacho tulikizungumza humu na Waziri akatoa kauli kwamba zoezi hilo linasitishwa, lakini jana tu wameuzwa ng'ombe zaidi ya 600. Kinachoendelea kule sio kwamba hata wale ng'ombe wanaokamatwa kwa sasa wanakamatwa kule hifadhini, wanafanya doria kwenye vijiji, wanawanyang'anya ng'ombe wanawapeleka mle, ukikosa hela wanapelekwa kwenye mnada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaotoka kwenye jamii ya wafugaji hasa Wasukuma wanaoonewa, tumechoka kuzika wazazi wetu ambao wanajiua baada ya kuuziwa ng'ombe zao. Tunataka kauli ya Serikali juu ya kuzuia minada ile kwa sababu mlalamikaji wa Mahakamani ni Serikali, Wizara ndiyo inalalamika kwamba ng'ombe zimekamatwa kule na anayeweza kuondoa ile kesi tufanye majadiliano mezani ni Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu ni nini kauli ya Serikali kuweza kuzuia zoezi lile tukae kwanza mezani, kwa sababu sisi kufuga hatukufuga kama laana hapa Tanzania, tumefuga kama wafugaji wanaofuga kwenye

mikoa mingine. Ni nini kauli ya Serikali kuzuia zoezi hili linalofanyika Kanda ya Ziwa kwa kauli itakayotoka humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimwia Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo. Nasimama kwa Kanuni ya 47, sitaisoma kwa sababu ya muda, hata hivyo kabla sijaenda kwenye mwongozo wangu nishauri pia wakati Mheshimiwa Jafo akiwa anajibu swali langu alinitambua kama Mbunge wa Masasi wakati mimi ni Mbunge wa Ndanda, kwa hiyo naomba irekebishwe. Hata hivyo wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais iliyofanyika Mtwara....

**MWENYEKITI:** Sasa huo ndiyo mwongozo unaouomba Mheshimiwa Mwambe?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Ndiyo! Sijamaliza.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la umeme katika Wilaya za Masasi, Mtwara kwa ujumla pamoja na Lindi na aliahidi kwamba kufikia tarehe 30 Mei tatizo hili litakuwa limekwisha na umeme utapatikana. Sasa kumekuwa na vifo vinatokea kwa akinamama kukosa huduma za upasuaji katika hospitali mbalimbali, lakini biashara nyingi zinafungwa kwa sababu ya kukosa umeme na ile ahadi haijatekelezwa mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Bunge lako liweze kujadili jambo hili kama suala la dharura ili wale wananchi waweze kuondokana na adha kubwa wanayoipata kwa sababu ukizingatia Mtwara na Lindi ndiko inakotoka gesi inayozalisha umeme Tanzania. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Mwongozo ninaouomba kutoka kwako ni kwamba, tunapopiga kura ya bajeti hatupigi tu kupitisha pesa ambazo tunataka kuruhusu Serikali itumie pesa na zikatumike kwenye Majimbo yetu. Tunapiga ile kura kwa kuonesha kwamba tunaiamini Serikali, ikusanye kodi vilevile kodi zile zirudi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yametokea wakati wa kipindi cha maswali na majibu kwa Naibu Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Uchukuzi, wameendelea kuonesha kana kwamba, kwa wale ambao tulipigia kura ya hapana Bajeti ya Serikali ni kama vile hatustahili kupata pesa ambazo zinakusanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaouomba kwako ni kwamba kama nilivyosema kura ile siyo tu kuidhinisha pesa, ni kura ya imani kwa Serikali iliyopo madarakani, naomba Bunge lielewe kwamba hapa hatujaja kwa *favour*, tuliwashinda kwenye Majimbo tuliyotoka. Kwa sababu tuliwashinda, wananchi wana imani na sisi, sasa ukisema zile pesa zisiletwe maana yake unasema kodi usiikusanye kutoka kwenye Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaouomba kinachofanyika katika Bunge hili hakipo popote katika Mabunge yote ya *Commonwealth*, hakipo popote kwenye *three lines Whip* duniani kama tunafuata utaratibu...

**MWENYEKITI:** Endelea na mwongozo Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninauomba ni kwamba, Je ni halali kwa Mawaziri kuendelea kudhalilisha *traditional way of doing Parliamentary practices* za *Three Line Whip* na kutaka kutuonyesha tuonekane *inferior* katika nyumba hii wakati tumekuja kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nami nasimamia Kanuni ya 47(1) nitakuomba pia na wewe unipatie ruhusa ya kutoa hoja kwa kuzingatia Kanuni ya 47(3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeboresha utaratibu wa kupima wagonjwa katika Hospitali ya Muhimbili na kwamba utaratibu mzima wa kupima mpaka kutoa majibu sasa hivi umekuwa *computerized,* kwamba kila kitu kinafanyika kwa kupitia *computer* na majibu yanatoka kupitia njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ya kukatika katika kwa umeme na inaonekana hakuna *standby generator* hasa kwa hizi wodi ambazo wananchi wetu wapiga kura wa kawaida ndiyo huwa wanalazwa, nina maana ya Wadi za Sewahaji, Kibasila, Mwaisela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hospitali hiyo hiyo tatizo hili la umeme haliliathiri ule upande mwingine wa *fast track.* Mgonjwa anaweza kufika pale amezidiwa akachukuliwa vipimo lakini akakaa siku mbili kusubiria majibu kwa sababu ya tatizo la umeme. Wako watu wamepoteza maisha, pia inaleta simanzi kubwa pale ambapo umetoka na mgonjwa mkoani amepewa rufaa, afike pale, akifika pale anakaa siku mbili bila kupata vipimo kwa sababu tu ya tatizo la umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linatugawa sana na linaonesha kama vile kuna tofauti ya nafsi ya mtu mwenye fedha na nafsi ya mtu ambaye hana fedha, kwamba maskini anaweza kupoteza maisha yake, tajiri anaweza akaokolewa maisha yake. Naomba Bunge lako leo litenge muda kidogo

tuweze kujadili mazingira haya ya utoaji huduma za afya katika hospitali yetu ya Muhimbili kwa maslahi mapana ya umma. *(makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

**MWENYEKITI:** Kanuni ipi?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 68(7), wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali la Wizara ya Fedha alikanusha kwamba Tanzania haiongozi kwenye viwango vya juu vya kodi katika *East Africa*. Ripoti ya Benki Kuu inaonesha hivyo ya mwaka huu, ripoti ya *PricewaterhouseCoopers* ya mwaka huu inaonyesha hivyo. Benki Kuu walienda mbele zaidi wakaonesha kwamba kwenye suala la *easy of doing business* Tanzania bado tuna tatizo kwenye *access to financing* na *tax rates* (viwango vya kodi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba endapo nikikuletea ushahidi hapo mezani Waziri atakuwa tayari kuwajibika kwa sababu amelidangaya Bunge lako Tukufu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mwongozo niliokuwa nataka kuuomba umeombwa na Mheshimiwa Peter Msigwa, kwa manufaa ya Bunge tungependa ufafanuzi utolewe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hebu rudia tena.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo niliokuwa nataka niombe, umeombwa na Mheshimiwa Msigwa, kwa manufaa ya Bunge hili na upotoshaji unaoendelea ni vizuri ufafanuzi utolewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Devotha, jiandae Mheshimiwa Kanyansu na Mheshimwa Mbarouk.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 46. Wakati nikiuliza swali kuhusu tatizo la ukosefu wa vifaa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa akijibu kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini. Hospitali ya Mkoa wa Morogoro iko *purposely* kwa ajili ya kusaidia Wilaya zote ambazo wagonjwa wanashindikana wanapelekwa katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro na Hospitali ya Mkoa wa Morogoro siyo Hospitali ya Jimbo wala siyo Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata mwongozo wako maana yake sasa imekuwa ni tabia kwa Manaibu Waziri wakijibu maswali wanajaribu ku-*relay* kwa Wabunge wa Majimbo badala ya ku-*focus* kwenye maswali ya msingi ambayo tunauliza kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ni kwa nini Waziri anaacha kujibu maswali *straight* anaanza kuleta siasa kwenye majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kanyansu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1)-(4) kama itakupendeza. Mji wa Geita ambao una wakazi takribani 100,000 ulikuwa unatumia maji ya bwawa la Nyankanga ambalo *catchment* yake ni eneo ambalo kuna maeneo mengi ya wachenjuaji wa madini na sasa limekauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza katika Bunge hili *capacity* ya maji katika Mji wa Geita ni asilimia tano hadi asilimia 10 na yanatolewa kwa mgao. Taasisi nyingi hazina maji na hali ni mbaya, kwa sababu

tulikuwa na mvua kidogo Kanda ya Ziwa visima vingi vimekauka na maeneo ya miji ya Kasamwa ambapo palikuwa na mabwawa yamekauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kwa kuwa hali hii baada ya mwezi mmoja Mji wa Geita utakuwa na hali mbaya sana, ni nini juhudi ya Serikali kuokoa hali hii au ichukue suala hili kama dharura kuhakikisha kwamba inaunga mkono juhudi za Viongozi wa Mkoa ambao wamewaomba watu wa mgodi wa *GGM* kuweka bomba dogo na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika baada ya miezi mitatu kuupatia maji ya dharura Mji wa Geita pamoja na mipango mizuri ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) na mwongozo wangu ni kama ifuatavyo:-

Wakati Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Mwakyembe akijibu swali la Mheshimwia Joseph Mbilinyi (Sugu) alitoa taarifa kwamba yaliyotokea katika chombo cha habari cha *TBC* yalikuwa ni mambo ya kawaida. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi alitaka kujua tu kwamba Watangazaji walitangaza uwongo kupitia *TBC* kwamba Rais Trump ampongeza Magufuli.

Mheshimiwa Waziri amelichukulia kama kitu kidogo akasema ni jambo la kawaida, lakini kutumia chombo cha habari kama *TBC* siyo jambo zuri linaweza likaleta mvurugano na wamerudishwa kazini wafanyakazi wale bila kuchukuliwa hatua, hata kupewa barua ya onyo. Je, kwa mfano, Watangazaji wale wangetangaza kwamba Rais Trump amtaka Mheshimiwa Rais Magufuli amtangaze Maalim Seif kuwa Rais halali wa Zanzibar, wangerudishwa kazini bila ya kuchukuliwa hatua? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ilikuwa ni jana hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Mavunde ana wageni 13 watangazaji na wafanyakazi wa Redio *AFM* ya hapa Dodoma, karibuni Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge nimepokea miongozo ya Wabunge kadhaa na karibuni miongozo mingi iliyoletwa hapa siyo mambo ambayo yametokea Bungeni kwa mujibu wa Kanuni zetu. Waheshimiwa Wabunge subirini, lakini kwa kitumia Kanuni ya tano (5) yapo mambo ambayo hayakutokea leo lakini yapo mambo ambayo yanawagusa watu. Hii ndiyo sehemu ya Mbunge kuweza kupumua na kuweza kufikisha ujumbe wa wananchi wake.

Mheshimiwa Musukuma suala la ng'ombe ni suala ambalo naiomba Serikali mjaribu kulitafutia ufumbuzi. Najua Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaanza kulifanyia kazi na naamini atalimaliza. Ni kweli Waziri wa Maliasili na Utalii alitoa *commitment* Bungeni kwamba hili suala litakwisha lakini linaendelea kuwepo.

Ni kweli watu wananyanyasika na ni kweli watu wananyang'anywa ng'ombe na ni kweli bora hao ng'ombe wangeuziwa wale ambao wamenyang'anywa lakini matokeo yake wanaletwa watu wengine kuja kununua hawa ng'ombe. Naamini Serikali mmelisikia na naamini Waziri Mkuu atalimaliza, kwa hiyo hili jambo sasa tuiachie Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Cecil Mwambe kuhusu suala la umeme nakuagiza uonane na Mheshimiwa Waziri mli-*sort out* ili muweze kulimaliza.

Mheshimiwa Peter Msigwa ninakurejesha kwenye Kanuni ya 53(8) ndiyo mwongozo wangu, jisomee mwenyewe nyumbani au baadaye hapo. Soma Kanuni 53(8) jambo ambalo limeshafanyiwa maamuzi jana au juzi na Bunge halitakuwa na nafasi tena ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Abdallah Mtolea jambo lako vilevile siyo jambo la kusitisha Bunge, lakini lina umuhimu kwa huduma

za hospitali zinasuasua kutokana na umeme. Nakushauri nawe uonane na Waziri ili muweze kuli-*sort out* ili huduma za umeme ziwe vizuri katika Hospitali ya Muhimbili.

Mheshimiwa Jesca Kishoa Bunge linapokea ripoti za Serikali na ndiyo sahihi, ripoti zingine ambazo zinakuja nje ya utaratibu wa Kiserikali Bunge hili hatuwezi kuzi-*entertain*. Kuna ripoti za mitandao, kuna ripoti nyingi ambazo hazijapata uthibitisho sahihi. Kama wewe una ripoti unaona ina umuhimu mpelekee Waziri wa Fedha aiainishe ya kwako wewe na ya kwake yeye halafu tupate suluhisho moja.

Mheshimiwa Devotha Minja Waziri wa Afya kumpongeza Mbunge aliyefanya mambo mazuri kwenye Jimbo siyo vibaya. Serikali inapongeza Wabunge hata upande wa Upinzani kwa kufanya mambo mazuri, ni jambo la kawaida tu Mbunge kupongezwa. Hana maana kuwa Mbunge wa Jimbo ndiye peke yake anayestahili kupongezwa. Leo hii hapa Serikali imempongeza Mbunge kutoka upande wa Upinzani kwa jitihada zake za kufuatilia mambo ya wananchi wake, kwa hiyo, mambo mengine siyo lazima myalete hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kanyasu ni kweli tatizo la maji lipo Geita, na natumia kanuni ya tano (5) hiyo *respect* za Mabunge ku-*entertain* na kukubali hoja yako. Nakuagiza sasa uonane na Waziri wa Maji ili muweze kulitazama vizuri na Waziri wa Mazingira ili kuhakikisha madhara haya hayawapati tena wananchi wetu.

Mheshimiwa Mussa Mbarouk nafikiri ulitaka tu kusherehesha Bunge, hawa watu wameshasamehewa siku nyingi na kesi hii imefungwa, kwa hiyo mwongozo wako siwezi kuujibu.

Mheshimiwa Hussein Nassor ana wageni wake Saba kutoka katika Jimbo lake la Nyang'hwale, wageni wa Mheshimiwa Hussein Nassor hebu simameni naye awaone. Karibuni na msiondoke jioni leo kuna futari hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo na *bonus* za maswali nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 5.40 Asubuhi Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kuna Mheshimiwa Mbunge au mwananchi yeyote aliyepoteza miwani yake anaombwa awasiliane na Makatibu Mezani, nafikiri ilisahaulika kwenye futari jana.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo lingine muhimu; kwa mujibu wa *Order Paper* yetu ya leo muda huu ilitakiwa Waziri wa Fedha na Mipango awasilishe maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 *(The Finance Bill 2017)* na kisha kuendelea na mjadala utakaofuatiwa na maoni ya Kamati ya Bajeti na maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati ya Bajeti kwa Muswada huu yamekuwa mengi kiasi ambacho Muswada huu umelazimika kuchapwa upya.

Kwa mantiki hiyo, Kamati inatakiwa kupitia tena ili kujiridhisha kwamba yale waliyokubaliana na Serikali yameingizwa katika Muswada huo. Kwa sababu, hiyo shughuli ya kupokea na kujadili Muswada huu haitaweza kufanyika leo. Hivyo baada ya matangazo yaliyopo mezani kwangu nitaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Alhamisi tarehe 22 Juni saa tatu asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, mmeuona umuhimu wa Kamati ya Bajeti ,namna inavyo-*engage* Serikali na Serikali hii sikivu tunavyosema na mambo mengi yamekubaliwa ndani ya maoni ya Kamati ya Bajeti na sasa hivi yanafanyiwa

kazi. Kwa hiyo, Kamati ya Bajeti iko *in session* na siyo vibaya kama kuna Mbunge ana hoja hakatazwi kwenda kwenye Kamati ya Bajeti akasikiliza na jambo lake linaweza likaishia kule kabla halijaletwa humu ndani.

Muswada mpya unagawiwa kwa Wabunge wote ili mkaupitie vizuri, kesho tuanze kazi kamili ya kuujadili na kuupitisha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 10.03 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamis, Tarehe 22 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*